# Nipashe

Jumatatu Machi 29, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580534

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710



Nipashe Spotika

WACHEZAJI 7 LIGI KUU BARA WALIOTESA KUFUZU AFCON... UK 14

NYOTA WATANO WANAOWEZA KUUZWA JUVE MAJIRA YA JOTO

UKURASA 11

**CAG:** Shirika la Ndege linajiendesha kwa hasara

UK. 4, 18



**TAKUKURU** yakamilisha uchunguzi majalada 1,079

UK. 5

# Samia aanza kwa kishindo

**Amsimamisha** Mkurugenzi Mkuu Bandari, ataka uchunguzi BoT, ainyooshea kidole TAMISEMI...*Endelea Uk. 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akimsikiliza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, wakati akitolea maelezo moja ya taarifa katika ripoti ya ukaguzi, Ikulu jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**MATUKIO UHALIFU, UTAPELI KINONDONI**

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoa wa kipolisi Kinondoni, Ramadhani Kingai, amesema katika mkoa huo kuna matukio ya utapeli na wizi wa mali na magari ya raia.

UKURASA WA 18

**WENGI WAJITOKEZA KUPIGA KURA PEMBA**

WANANCHI wa Jimbo la Pandani Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba, jana, walijitokeza kupiga kura katika vituo 18 vilivyomo katika uchaguzi mdogo wa kujaza nafasi ya aliyekuwa mwakilishi mteule ...



## Mtangazaji ITV auawa kinyama Dar

UKURASA 4



## ...Jafo awageukia waweka hazina, wakaguzi wa ndani

UK. 3

**MICHEZO** BARAZA ATAJA SHIDA ILIPO KAGERA SUGAR UK.23 | **MAONI, KATUNI** UK.6

## CAG: Shirika la Ndege lajiendesha kwa hasara

**Na Elizabeth Zaya**

MKAGUZI na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, amesema kuwa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) mwaka 2019/2020 limejiendesha kwa hasara ya Sh. bilioni 60.

Aidha, alibainisha kuwa kwa miaka mitano mfululizo ATCL inajiendesha kwa hasara.

Akiwasilisha ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2019/2020, jana Ikulu ya Chamwino, jijini Dodoma kwa Rais Samia Saluhu Hassan, alisema kwa ujumla shirika hilo limekuwa likijiendesha kwa hasara kwa miaka mitano tangu 2015.

Pia CAG alimkabidhi Rais Samia ripoti 21 za mashirika na taasisi za umma kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020.

"Kwa mwaka huu tumebaini kwamba ATCL imetengeneza hasara ya Sh. bilioni 60 na imekuwa ikitengeneza hasara kwa miaka mitano. Tumebaini kwamba kuna changamoto mbalimbali ambazo serikali inabidi iziangalie ili shirika litekeleze majukumu yake vizuri bila hasara," alibainisha Kichere.

**UCHAKACHUAJI TEHAMA**

CAG amesema wamebaini matatizo na kuisababishia serikali hasara ni pamoja na mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

"Katika TEHAMA, tumekagua na kugundua kuna mifumo mingine ambayo 'security' (usalama) yake siyo nzuri, kuna mianya kadhaa ambayo inaweza kusababisha upotevu wa fedha katika kuitumia, kwa hiyo ni vyema serikali ikaiangalia ili tupate udhibiti na kuhakikisha mapato yanayokusanywa yanaingia ndani ya serikali na hakuna uvujaji," alisema Kichere.

"Tunakusanya mapato mengi, lakini sehemu kubwa ya mapato hayo yanavuja kutokana na mifumo tunayoitumia," alisisitiza.

**TPA**

CAG aliitaja Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), kuwa ni miongoni mwa taasisi za umma ambazo zimekutwa na changamoto.

"Tumegundua matatizo kadhaa kwenye shirika letu la Bandari ikiwamo ubadhirifu ambao pia tunaendelea kufanya ukaguzi kwenye maeneo hayo, na tunaomba serikali ichukue hatua," alisema Kichere.

**RIPOTI KUPELEKWA BUNGENI**

Alisema ipo ripoti ndogo yenye mambo muhimu ambayo baada ya rais kuipitia itapelekwa bungeni na baada ya hapo kuwekwa hadharani kwa umma.

"Katika ripoti yangu, kuna mambo mengi ya msingi ambayo nimekagua na ambayo nimetolea mapendekezo. Pia nitakukabidhi ripoti ndogo ambayo kuna mambo muhimu ambayo naona kwamba ni vyema Rais ukayaelewa, nitakuomba uisome hiyo ripoti yangu ndogo, uone ni nini kipo," alisema Kichere.

"Na ripoti hiyo ikishafika ndani ya Bunge itakuwa 'public' (umma), kwa sababu kabla haijafika inakuwa haiko public. Lakini nimeamua nikuambie hizo changamoto ili ikiwezekana uchukue hatua za haraka kupitia hiyo taarifa yangu."



Rais Samia Suluhu Hassan akimsikiliza Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kupambana na Rushwa nchini, Brigedia Jenerali John Mbungo, wakati akitolea maelezo moja ya taarifa zake za ripoti ya kuzuia na kupambana na rushwa kwa mwaka 2019/20, Ikulu jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Samia aanza kwa kishindo

**Na Salome Kitomari**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameanza kuonyesha makali yake kwa kumsimamisha kazi Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Mhandisi Deusdedit Kakoko, kwa tuhuma ubadhirifu wa Sh. bilioni 3.6 uliotokea ndani ya mamlaka hiyo, ili kupisha uchunguzi.

Ikiwa ni hotuba yake ya pili kwa taifa baada ya kuapishwa Machi 19, mwaka huu, kuwa Rais wa sita wa Awamu ya Tano, Rais Samia jana, alipokuwa akipokea ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa mwaka 2019/2020.

Katika hotuba hiyo ya pili, makali yake yalionekana baada ya kutamka kumsimamisha kazi mkurugenzi huyo na kuagiza kufanyika uchunguzi wa kina dhidi ya wote waliohusika, uchunguzi wa fedha zilizotoka na kuingia Januari hadi Machi, mwaka huu Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na upotevu wa fedha katika halmashauri.

"Katika ripoti yako (CAG) nimeona ubadhirifu mkubwa bandarini, naomba TAKUKURU hii ni special (maalum) kazi jishughulishe pale (TPA), najua Waziri Mkuu aliunda kamati na wakafanya uchunguzi kidogo pale na mambo yaliyotoka hatua chache zilizochukuliwa," alisema na kuongeza:

"Imani yangu ni kwamba kama kuna ubadhirifu ndani ya shirika na kwa ripoti uliyonikabidhi kuna ubadhirifu wa Sh. bilioni 3.6 karibu Sh. bilioni 4, lakini wakati Waziri Mkuu amefanya ukaguzi waliosimamishwa ni watu wa chini, naomba mara moja kutoa agizo la kumsimamisha Mkurugenzi Mkuu wa TPA wakati uchunguzi unaendelea."

Alisema uchunguzi huo utafanyika hadi kwenye mashirika mengine kama ATC na mengine na ndipo maamuzi ya pamoja yatafanyika.

**ATAKA UCHUNGUZI BoT**

Aidha, Rais Samia ambaye ni mwanamke wa kwanza kuwa rais Afrika Mashariki, alimwagiza CAG kushirikiana na Gavana wa BoT, kupitia fedha zote zilizotoka BoT kuanzia Januari hadi Machi, mwaka huu na kumkabidhi ripoti.

**TAMISEMI KIKAANGONI**

Rais Samia alisema TAMISEMI kuna upotevu mkubwa wa fedha na wanafanya kama vile sheria zinazotungwa kwenye serikali kuu haziwahusu.

"Na hili Hayati John Magufuli alishakwambia (Waziri Selemani Jafo) mara mbili, mara tatu, naomba ukasimamie mapato na matumizi ya TAMISEMI, hangaika mara ya mwisho ukishindwa tuambie tukusaidie, lakini hali hairidhishi TAMISEMI," alisema na kuongeza:

"TAMISEMI wanachukua fedha nyingi serikali kuu, lakini wao wanakula hawarudishi, naomba simamia hilo, fedha zinazokusanywa zisipotee na zinazokwenda zitumike zinavyostahiki."

Rais Samia alisema mawaziri wanapaswa kusimamia maeneo yote yenye upungufu yaliyojitokeza kwenye ripoti ya CAG, huku akitaka TAKUKURU kukaa na CAG kuangalia mifumo ya malipo zaidi ya sita inayotumika kukusanya mapato sehemu mbalimbali.

"Naomba mwangalie mifumo, tuangalie ndani ya serikali mifumo gani inatumika na ukusanyaji wake ukoje, maana mifumo ikiwa mingi unatoa mwanya wa kupoteza mapato, ijulikane kama ni mitatu inayotumika kukusanya, kutoa na matumizi ya fedha za serikali," alisisitiza.

Aidha, alisema kama ni taaluma mpya waseme kama haiwezekani watafutwe wataalamu kutoka nje kusaidia kuwa na mifumo michache yenye ufanisi.

**ATAKA CAG KUKUNJUA MAKUCHA**

Kuhusu mashirika ya umma, CAG naomba sana ulimi wako usiwe na utata, kama kuna shirika halifanyi vizuri tuambie, kama bodi haisimami vizuri tuambie, tutakaposema upungufu ndipo tutaweza kurekebisha na kuweza kufanya vizuri zaidi, tukinyamaziana kwa kutizamana sura, hatutarekebisha na tutawaumiza wananchi," alisema.

Aidha, aliagiza uwazi katika ripoti ya mashirika ya umma, na kwamba atakapoipeleka mezani kwake ahahakikishe iko wazi ili kujua hatua za kuchukua.

Kwa mujibu wa Rais Samia, kwenye Mashirika ya Umma hakuna hati chafu wala zisizoridhisha lakini upotevu mkubwa unatokea huko, na kwamba hali siyo shwari na hatua za haraka zinatakiwa kuchukuliwa.

**ATAKA TAKUKURU KUFUTA KESI**

Kuhusu ripoti ya TAKUKURU, aliitaka taasisi hiyo kufuta kesi ambazo wanaona hawana misingi mizito ya kushinda kabla ya kuzipeleka, kwa kuwa kila siku kusoma kuna kesi 300 ziliplekwa mahakamani na zilizoshinda ni 130 au zaidi haileti sura nzuri kwa serikali, huku akiwataka kuongeza kiwango cha ushindi wa kesi ili kuleta heshima ya serikali. "Nawapongeza kwa kuongeza kiwango cha kushinda kesi kufika asilimia 9.67 na nyingi tunashindwa kwa sababu hazikuwa na misingi mizuri ya kubambikiza. Nakuomba utazame vizuri kesi zozote unazohisi huna misingi mizito ya kushinda zifute kabla hujafika huko (mahakamani)," alisema.

Aidha, Rais Samia alitaka kupitiwa upya sheria za kuwalinda mashahidi na watoa taarifa ikiwamo kuangalia watendaji ambao wanavujisha siri kiasi cha kutengeneza visasi na kutafutana mtaani.

"Kwa sasa bado mashahidi hawajalindwa vizuri ni muhimu sana kuliangalia, yawezekana kuna udhaifu kwenye ofisi yako (TAKUKURU)," alisema.

Kuhusu urudishaji wa madeni, alitaka kuangaliwa kwa mfumo mwingine wa mashirika yanayodai kurudishiwa mali zao kwa kuwa TAKUKURU kuingia huko ni kutoka kwenye eneo lao, kama deni limetokana na rushwa ni sawa lakini kama ni madeni ya shirika lililotoa huduma na hawarudisha hakuna rushwa bali ukakasi wa kukusanya madeni.

**RUSHWA YA NGONO**

Rais Samia aliwataka kupanua utafiti huo hadi vyuo 64 vilivyopo nchini ikiwa ni pamoja na kwenda mbali zaidi kuangalia rushwa za uvujishaji mitihani na nyingine ambazo zinaikabili sekta hiyo.

**NITASIMAMA IMARA**

Aidha, Rais Samia aliwaonya watumishi wa umma wanaotumia vibaya ofisi za umma kuacha mara moja na kwamba atasimama imara kwenye makusanyo na matumizi ya fedha za serikali na mapambano dhidi ya rushwa.

"Waliopo kwenye taasisi za umma, mashirika ya serikali na binafsi, naomba tufuate maadili ya kazi, taasisi na sheria ili kurahisisha kazi ya CAG na TAKUKURU," alisema.

HABARI KITAIFA

# Jafo awageukia waweka hazina, wakaguzi wa ndani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amemwagiza Katibu Mkuu wa ofisi hiyo, Mhandisi Joseph Nyamhanga, kuwaondoa katika nafasi zao waweka hazina na wakaguzi wa ndani wa halmashauri nane zilizopata hati chafu. Aidha, amesema atawasilisha majina kwa Rais Samia Suluhu Hassan ya wakurugenzi wa halmashauri hizo kwa ajili ya kutoa uamuzi huku akiwataka wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa kujitathmini. Hatua hiyo, inatokana na ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2019/20, iliyowasilishwa jana kwa Rais Samia. Akizungumza na waandishi wa habari jana, Waziri Jafo alisema ofisi yake imejipanga kuchukua hatua kali kwa halmashauri hizo.

"Namwagiza Katibu Mkuu kuanza kufanya uchambuzi wa taarifa hiyo na kuwatengua wale wakaguzi wa ndani maana nilitarajia jukumu lao kubwa ni kusimamia mwenendo wa fedha, kama yupo na inaonekana halmashauri yake inafanya vibaya inamaana ameshindwa kushauri vizuri halmashauri yake, naagiza awaondoe kwenye nafasi zao mara moja baada ya uchambuzi wa taarifa hiyo," alisema.

"Wawekahazina ni watu muhimu kuhakikisha utaratibu wa fedha na miongozo mbalimbali ya kifedha, yeye ndiye mshauri mkuu na msimamizi, namwelekeza Katibu Mkuu Nyamhanga katika halmashauri hizo nane ahakikishe tunaweka watu wazuri kwenye nafasi hizo."

Alisisitiza Katibu Mkuu huyo achukue hatua si kwa kubembelezana bali kutengua nafasi zote za viongozi hao. Kuhusu wakurugenzi, Jafo alisema; "Sijaridhika kabisa licha ya kutoa mafunzo mbalimbali na maelekezo ya usimamizi na udhibiti wa fedha, lakini wakurugenzi hao wameonyesha halmashauri zao zimefanya vibaya, hiyo kwa sababu wakurugenzi mamlaka zao za uteuzi ipo kwa rais, nitawasilisha majina yao."

Waziri Jafo alisema atawasilisha majina hayo ili mamlaka hiyo itoe uamuzi kwa kadri itakavyoona inafaa. "Namwagiza Katibu Mkuu TAMISEMI achambue vyema taarifa hiyo kwa kina na kwenda kubainisha watu wengine wote waliotajwa kwenye taarifa ya CAG kwenye halmashauri ambazo zipo nje ya hizo nane, ambazo zimeguswa kwamba katika mwenendo hata kama umepata hati safi," alisema.

# 2 wasubiri baraka CCM, ACT Kibondo

**Na Deogratius Nsokolo,** KIBONDO

MFANYABIASHARA na kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Kibondo, Mkoa wa Kigoma, Jamal Abdalah Tamim, ameibuka mshindi wa kura za maoni ndani ya chama hicho kuelekea kumpata mrithi wa aliyekuwa mbunge wa Muhambwe, Atashasta Nditiye, aliyefariki Februari 12, mwaka huu jijini Dodoma.

Abdalah amepata kura 137 na kuwashinda wagombea wenzake 24 alioingia nao katika kinyang'anyiro hicho ambapo amefuatiwa na Dickson Bidebeli aliyepata kura 132 na Dk. Florence Samizi (78), huku aliyewahi kuwa mbunge wa jimbo hilo mwaka 2005-2010 na mkuu wa mkoa wa zamani wa Arusha, Felix Kijiko akiambulia kura 23.

Akitangaza matokeo hayo, mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Kigoma, Thomas Sangai, aliyesimamia kura za maoni katika jimbo hilo alisema jumla wa wapigakura ambao ni wajumbe 484 walishiriki. Alisema baada ya matokea hayo ya kura za maoni, vikao vya juu ya chama vitarejesha jina moja la atakayeteuliwa kugombea nafasi hiyo katika uchaguzi mdogo wa ubunge Jimbo la Muhambwe utakaofanyika Mei 2, mwaka huu.

Wakati huohuo, Chama cha ACT-Wazalendo katika wilaya ya Kibondo kimepitisha jina moja la Julius Joseph Masabo kuwa mgombea wa chama hicho katika uchaguzi huo, baada ya kuwa mgombea pekee.

Katibu wa ACT wilayani Kibondo, Sixbert Bunyambo, alisema kutokana na kujitokeza mwanachama mmoja, hakuna kura za maoni na badala yake jina hilo limepelekwa katika vikao vya ngazi za juu.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GEORGE FANUEL MAKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **TVS** yenye namba za usajili **MC 722 CLH** Chassis **No.MD625AF48k1k06280**, Engine No.**Df4kk1905958**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **GEI/BUK/RB/138840/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI**
**SONGWE-VWAWA**
**SHAURI LA MADAI NA 4 YA 2021**
**CRDB**
**VS**
**KULWA ERASTO KACHE**

**Kwa: KULWA ERASTO**
**POPOTE ULIPO**

**Kuitwa shaurini mdaiwa.**

Unataarifiwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa mahakama ya Wilaya ya Mbozi tarehe 30/03/2021, siku ya Jumanne saa 3:00 asubuhi,ambapo shauri limepangwa kutajwa.

Elewa kwamba ukikosa kufika siku hiyo shauri litapangwa kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 12/03/2021.

**HAKIMU**




NORWEGIAN CHURCH AID
actalliance

## Advertisement of Business Opportunities

**Date: 29th March 2021**

**Reference no: 0001/NCA/2021**

**Subject: Consultancy Service**

**Contracting Authority: Norwegian Church Aid - Tanzania Office**

**Deadline for submission of letter of interest: 5th April 2021**

**Background**
Haydom Lutheran Hospital (HLH) was established in 1955 and has since practiced a holistic approach to health care for its patients, to meet the "total needs of the person" (spiritual, social, and health needs). The hospital is in Northern part of Tanzania around 300km from Arusha. HLH is a Faith Based Hospital owned by Evangelical Lutheran Church of Tanzania (ELCT) Mbulu Diocese and works in partnership with Government of Tanzania. HLH operates as a regional referral level hospital for the purpose of delivering quality health services in Manyara and nearby regions, having 420 bed capacity and approximately 500 staff. This hospital has long term partnership with Norwegian Government in funding through The Norwegian Agency for Development Cooperation (NORAD), Royal Norwegian Embassy (RNE) and Norwegian Church Aid (NCA).

NCA invites qualified and experienced applicants to respond to this advertisement.
Applicants who have responded to this advertisement and provided the required information may be invited to participate in the procurement procedure for the relevant lot(s).

**Service required:**
**Midterm Evaluation of the project - Haydom Lutheran Hospital 2019-2022**

The service relates to a project, which seeks to improve, among others the quality of health services and foster organizational development of the hospital. The interested applicants shall provide the following information preferably **in one page** to the Contracting Authority using the contact details below:

- The company's name and contact details.
- Contact person.
- A brief description of the company's background and main line of work.
- A brief description of the company's experience in evaluations, health facility management and organisational development.
- A minimum of 5 years of experience with this kind of service

This is purely information on business opportunities and **does not** constitute a commitment to purchase or any other form of contractual commitment with the Contracting Authority.

Information should be provided to the following address by email:

**Country Director,**
**Norwegian Church Aid**
**Plot 436, Mikocheni II Mwai Kibaki Rd,**
**Dar es Salaam, Tanzania+255 22 2 700 252**
**e-mail: Procurement.Tanzania@nca.no**

# ACT-Wazalendo yasisitiza wananchi ushirikiano

Na Mwandishi Wetu

KIONGOZI Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amewataka wananchi kuendelea kushirikiana, kuendeleza mapambano ya kudai haki na kuendeleza ndoto ya aliyekuwa Mwenyekiti wa chama hicho, Maalim Seif Sharif Hamad ya kuwa na Zanzibar yenye umoja, maridhiano na maendeleo.

Aliyasema hayo huko kisiwani Pemba wakati wa dua maalum ya kumwombea Maalim Seif aliyefariki Februari 17, mwaka huu na juzi akiwa ametimiza siku 40 tangu alipofariki dunia.

Alisema kwa sasa wanaendelea vizuri kuishi katika umoja na mshikamano na akataka kuendelea na kasi hiyo.

"Kwa hakika hadi sasa tunakwenda vizuri tunamshukuru Mungu endeleeni na dua zenu na penye mikwamo tutakuja kulizungumza, lakini mpaka sasa tunaendelea vizuri hakuna mkwamo wowote," alisema.

Alisema bado wana deni kwa wananchi la kupigania haki licha ya Maalim Seif muda wote kuwa katika mapambano ya kudai haki.

Naye Mkurugenzi wa Mawasiliano na habari wa chama hicho, Salum Bimani, alisema wataendelea kushirikiana na serikali kumuenzi na kumkumbuka Maalim Seif na kutekeleza yote mazuri aliyokuwa akiyafanya ikiwamo suala la maridhiano.

"Bado tunaendelea kumkumbuka kiongozi wetu Maalim Seif Sharif Hamad, Mungu amlaze pahala pema peponi," alisema Bimani.

Alisema licha ya chama kuondokewa na kiongozi huyo, watahakikisha chama kinasonga mbele na kushirikiana na serikali kuiletea



Baadhi ya wapigakura katika kituo cha Kiungoni Wilaya ya Wete, wakisubiri kupiga kura zao kwa ajili ya uchaguzi mdogo unaofanyika katika Jimbo la Pandani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtangazaji ITV auawa kinyama

Na Christina Mwakangale

JESHI la Polisi Mkoa wa Kinondoni, limesema uchunguzi wa awali umebaini kuwa kifo cha aliyekuwa mwandishi wa habari wa ITV/Radio One na mtangazaji wa kipindi cha Jarida la Wanawake, Blandina Sembu (47) (pichani), kimetokana na kuuawa kwa kupigwa na kitu chenye ncha kali usoni.

Uchunguzi huo pia umebaini mazingira yalikofanyika mauaji ya Blandina, hayalingani na mwili ulikookotwa eneo la Bamaga-ITV, Mwenge, jijini Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi mkoa huo, Ramadhani Kingai, akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu tukio hilo, alisema mauaji hayo yalitokea usiku, Machi 27, mwaka huu.

"Niwajulishe kwamba tarehe 27, mwezi na mwaka huu, eneo la Maryland Bar, njia panda ya ITV, watu wasiofahamika wakiwa na gari aina ya Noah, (namba haijatambuliwa), walisimamisha gari eneo hilo, kwa muda mfupi na lilipoondoka ulipatikana mwili wa jinsia ya kike, uliotambulika kuwa ni wa Blandina Sembu (47), mfanyakazi wa ITV, Redio One," alisema Kamanda Kingai.

Alifafanua kuwa, marehemu alikuwa mkazi wa Zinga, Bagamoyo, mkoani Pwani.

Alisema baada ya tukio hilo Jeshi la Polisi limeanza uchunguzi wa kina zaidi.

Alisema uchunguzi wa awali unaonyesha eneo alikouawa Blandina na ulikookotwa mwili ni vitu viwili tofauti.

"Eneo alikookotwa ni Area B, alikouliwa ni kwingine, sababu mwili ulionekana muda mfupi tu eneo la Bamaga, hivyo uchunguzi unaendelea."

"Ni mauaji, kifo cha mashaka ni kweli amekuwa na majeraha usoni kidogo, ila kwenye jicho inaonekana alipigwa na kitu kizito, si kifo cha kawaida. Wataalamu wetu wapo 'field' (kazini), maana eneo alikookotwa marehemu siko alikouliwa pale aliendа



kuwekwa tu."

"Magari yalivyokuwa yanapita mita 200 toka mwili ulikotupwa, walipoenda kuangalia wakaukuta mwili wa mwanamke, na kutoa taarifa. Ni tukio la mauaji ambalo linaonyesha marehemu alipigwa na kitu kizito chenye ncha kali."

# Matukio ya uhalifu, utapeli Kinondoni

Na Christina Mwakangale

KAMANDA wa Jeshi la Polisi mkoa wa kipolisi Kinondoni, Ramadhani Kingai, amesema katika mkoa huo kuna matukio ya utapeli na wizi wa mali na magari ya raia.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema lipo kundi la watuhumiwa ambalo hufanya matukio ya kudanganya na utapeli wa watu kujifanya maofisa wa polisi, watumishi wa serikali na kujipatia fedha isivyo halali.

Alisema Machi 23, mwaka huu, eneo la Mbezi Salasala, Mtaa wa Big Brother, Emmanuel Edward, alipatikana na simu za wizi.

Kamanda Kingai alisema mtu mwingine ambaye ni Mhasibu wa kampuni ya Famali Investment, aliyekuwa akitokea Benki ya Exim Kariakoo, aliporwa Sh. milioni 37.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, waporaji walikuwa wakitumia pikipiki na polisi walianza uchunguzi na kuwakamata watuhumiwa watatu na kuokoa Sh. milioni 24 kati ya fedha zilizoporwa.

"Watuhumiwa ni Bahati Musa, Mwinyi Ismail na Ally Masoud, ambaye alikuwa dereva wa mtu aliyeporwa. Dereva alisimama ghafla na mara watu wakavamia gari," alisema kamanda huyo.

Pia Machi 13, mwaka huu, watuhumiwa tisa walikamatwa kwa kujihusisha na utapeli ikiwamo kuwatishia watu. Kamanda Kingai alisema watuhumiwa hao walifika kwa Elias, wakidai anafanya biashara bila leseni na kumtaka awapatie shilingi milioni tano.

Kadhalika, kuhusu matukio mengine yaliyotokea mkoa huo, Kamanda Kingai alisema, watuhumiwa kadhaa walikamatwa kutokana na matukio tofauti huku Machi 23, mwaka huu, majira ya mchana eneo la Kisopwa, Allan Mushi (61), alikamatwa akiwa na silaha.

Kamanda Kingai alisema silaha aliyokamatwa nayo ni aina ya Mark 4 namba J 56289, iliyokuwa na risasi saba na bastola moja yenye risasi mbili. Pia aliongeza kwamba Machi 24, mwaka huu, eneo la Bunju B, polisi kwa kushirikiana na raia wema waliwakamata raia wa Somalia wanne walioingia nchini kinyume cha sheria.

Aliwataja raia hao kuwa ni Mohamed Ally (16), Abdukadir Mohamed (18) na Sharumake Adamu (18) na Khalid Bashiri (18).

"Baada ya mahojiano kukamilika watafikishwa Idara ya Uhamiaji kwa hatua za kisheria," alisema Kamanda Kingai.

Kamanda alisema Machi 14, mwaka huu, eneo la Kisunga-Madale, liliibiwa gari yenye namba za usajili T 920 DQX Toyota IST, nyeupe yenye thamani ya Sh. milioni 12 mali ya Isack Mhava, na baada ya uchunguzi jeshi hilo lilipata gari hilo eneo la Msongola na kwamba mmiliki alifuate kituo cha polisi.

HABARI KITAIFA

# TAKUKURU yakamilisha uchunguzi majalada 1,079

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imechunguza na kukamilisha majalada ya kesi 1,079 kwa kipindi cha mwaka 2019/20 zenye tuhuma mbalimbali ikiwamo ukwepaji kodi. Aidha, imebaini mambo manne katika halmashauri nchini kwenye mifumo ya ukusanyaji wa mapato ikiwamo watendaji kuchezea mifumo na kukwepa kutoa stakabadhi za kielektroniki.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo, Brigedia Jenerali John Mbungo, aliyasema hayo jana alipokuwa akitoa taarifa ya utendaji kazi wa taasisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/20 kwa Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu Chamwino.

Alisema taasisi hiyo imechunguza na kukamilisha majalada 1079 yenye tuhuma mbalimbali za ukwepaji kodi, matumizi mabaya ya fedha za umma, vyama vya ushirika wa masoko ya mazao ya kilimo kutokuwalipa wakulima, mikopo umiza, ufujaji wa fedha kwenye miradi ya maendeleo.

"Kati ya majalada hayo majalada 385 yalihusu hongo na majalada 94 yalihusu vifungu vingine vya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, majalada 443 yaliwasilishwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuombewa vibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani," alisema.

Aidha, alisema kwa kipindi hicho kesi mpya 586 zimefunguliwa katika mahakama mbalimbali nchini ambapo kesi 381 zilitolewa uamuzi na kesi 267 watuhumiwa walipatikana na hatia na kuhukumiwa vifungo au kulipa faini zikiwamo kesi tatu kutoka Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya rushwa na uhujumu uchumi.

"Zipo pia kesi nne zenye hadhi ya mahakama ya mafisadi zinazoendelea mahakamani, kiwango cha kushinda kesi kiliongezeka na kufikia asilimia 70.08 ikilinganishwa na asilimia 60.4 mwaka 2018/19," alisema.

Pia alisema taasisi imeokoa Sh. bilioni 96.02 kupitia operesheni mbalimbali ikiwamo Sh. bilioni 66.28 taslimu zilizorejeshwa kwa benki, taasisi na wananchi husika.

"Sh. bilioni 29.74 zimedhibitiwa na kuelekezwa kwenye ukamilishaji wa miradi ya maendeleo ili kutimiza matakwa yaliyokusudiwa," alisema. Alisema TAKUKURU imeweka zuio la mali za washtakiwa zenye thamani ya Sh. milioni 146.63, viwanja 13 na vyumba sita.

Kuhusu ushiriki kwenye vikosi kazi kutokana na matumizi mabaya ya fedha za umma, mkurugenzi huyo alisema kupitia kikosi kazi kilichoundwa na Katibu Mkuu Hazina, Sh. bilioni 60 zililipwa Hazina kama sehemu ya kodi iliyokwepwa na wafanyabiashara.

"Kiasi cha Sh. milioni 129.2 ziliokolewa na kikosi kazi kutokana na wizi wa mapato yanayotokana na utumiaji umeme, pia Sh. milioni 62.6 ziliokolewa katika kazi inayohusisha Makumbusho ya Taifa," alisema.

Kuhusu utendaji wa vyama vya ushirika, mkurugenzi huyo alisema imebainika kutokuwapo kwa uwazi na uwajibikaji, uhaba wa watumishi hasa wakaguzi, uwezo mdogo wa viongozi, kuwapo kwa rushwa. "Miradi ya maendeleo 1031 ilifuatiliwa kwa kipindi hiki yenye thamani ya Sh. trilioni 11.08, katika sekta za kipaumbele za afya, elimu, maji na ujenzi," alisema.

Aidha, alisema katika miradi iliyofuatiliwa 199 yenye thamani ya Sh. bilioni 174.4 ilibainika kuwa na viashiria mbalimbali ikiwamo viashiria vya ufujaji wa fedha, uchunguzi ulianza mara moja kwenye maeneo hayo.

Kuhusu mifumo ya ukusanyaji wa mapato, Mbungo alisema kutokana na uchambuzi wa mifumo ya ukusanyaji mapato uliofanywa na taasisi hiyo kwenye halmashauri zote na kubaini kutozingatiwa kwa ulipaji wa ushuru na ada mbalimbali.

"Watendaji kutotoa stakabadhi za kielektroniki, kukwepa matumizi ya mashine na kuchezea mifumo au mashine zisifanye kazi, udhaifu wa kufuatilia mashine kwenye mifumo pamoja na madiwani kutojadili masuala ya makusanyo ya mapato kwenye kamati za maendeleo ya kata," alisema.

Pamoja na hayo, alisema kwa mwaka 2019/20 TAKUKURU imetekeleza majukumu yake ya kupambana na rushwa kwa asilimia 89.8 tofauti na malengo ya mwaka 2018/19 ambapo ilikuwa asilimia 88.1.

"Ongezeko hili limetokana na kukamilisha uchunguzi wa majalada 1079, ikilinganishwa na majalada 911 yaliyokamilishwa kwa mwaka 2018/19," alisema.

Kuhusu miradi ya maendeleo, alisema taasisi hiyo imefuatilia miradi yenye thamani ya Sh. trilioni 11.08 ilifuatiliwa ikilinganishwa na miradi ya Sh. trilioni 1.67 iliyofuatiliwa kwa mwaka 2018/19.

Kuhusu ufuatiliaji wa fedha za Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC) Sh. bilioni 27.3 ambazo zimetolewa kwa ajili ya kukopesha wananchi matrekta, mkurugenzi huyo alisema mwaka 2018 NDC ilikopesha matrekta kwa wananchi na ndani ya miezi sita kuanzia Agosti 2020 hadi sasa imeokoa Sh. bilioni 2.08.

# UNHCR yasaidia kujikinga na magonjwa

**Na Deogratius Nsokolo,** KIGOMA

Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) limetoa msaada wa dawa na vifaa tiba vya kujikinga na maambukizi ya magonjwa mbalimbali ya kuambukiza ukiwamo COVID-19 na ebola kwa wahudumu wa afya mkoani Kigoma.

Mkuu wa hilo katika wilaya ya Kasulu, Ben Diallo, alikabidhi msaada huo wenye zaidi ya thamani ya shilingi milioni 100 kwa Mganga Mkuu wa mkoa wa Kigoma, Dk. Simon Chacha na kueleza kuwa unalenga kuimarisha huduma za afya nje ya kambi za wakimbizi.

Alisema shirika hilo linatambua umuhimu wake katika kuwahudumia wakimbizi na jamii ya watu wa Kigoma ambayo imepokea wakimbizi, hivyo itaendelea kusadia upatikanaji wa huduma za kijamii kwa wananchi katika sekta mbalimbali.

Diallo alisema agonjwa ya mlipuko kama COVID-19 ni hatari na vita yake inatakiwa kuwa endelevu katika jamii, hivyo vifaa hivyo vitasaidia katika kujikinga.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali isiuache Uwanja wa Magufuli kuwa gofu

**WATANZANIA** bado wapo katika kipindi cha maombolezo ya siku 21 baada ya kumpoteza aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, ambaye alifariki dunia Dar es Salaam kwa maradhi ya moyo Machi 17, mwaka huu na kuzikwa Ijumaa iliyopita nyumbani kwao Chato mkoani Geita.

Kwa hakika kumpoteza Dk. Magufuli ni pigo kubwa kwa maendeleo ya nchi yetu hususan sekta ya michezo ambayo kwa kipindi kifupi tu cha uongozi wake, tayari Watanzania wameshuhudia mabadiliko makubwa michezoni.

Hakuna ubishi kwamba katika utawala wa Dk. Magufuli, ndipo tumeshuhudia Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), likirejesha fedha za miradi ya maendeleo ya soka kwa Shirikisho la Soka nchini (TFF), baada ya serikali yake kuwa mstari wa mbele kudhibiti mianya yote ya rushwa na kuwachukulia hatua wote waliohusika na ufujaji huo.

Lakini katika kipindi cha uongozi wa Dk. Magufuli, kwa mara ya kwanza, tumeshuhudia serikali ikitangaza rasmi kuanza kuzihudumia timu zote za michezo za taifa, kitu ambacho hapo awali suala hilo liliachwa kwa mashirikisho na vyama husika.

Kwa upande wa soka, tumeshuhudia akiwa mstari wa mbele kuhakikisha miundombinu inaboreshwa kwa kupatikana viwanja vipya na bora, ambapo Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na ile ya Morocco, zimekubaliana kuwezesha kujengwa uwanja mkubwa kuliko vyote nchini katika Jiji la Dodoma.

Tayari kuna Uwanja wa Majaliwa unaotumiwa na Namungo FC, pale Ruangwa mkoani Lindi, ambao unaendelea kujengwa majukwaa ya kisasa, hizo zote zikiwa ni juhudi za serikali kuhakikisha miundombinu ya michezo inakuwa bora nchini ili kuzalisha ajira kwa vijana.

Katika juhudi hizo, pia serikali ya Dk. Magufuli ilianza ujenzi wa uwanja mkubwa wa kisasa Chato mkoani Geita, sehemu ambayo shughuli za kumuaga Hayati Dk. Magufuli zilifanyika kabla ya kwenda kupumzishwa katika nyumba yake ya milele, nyumbani kwao.

Tunatambua ujenzi wa uwanja huo ni sehemu ya miradi mikubwa ya soka ambayo Dk. Magufuli alitamani kuona Tanzania inakuwa na miundombinu bora kabisa na yakisasa katika sekta ya michezo ili kuzalisha ajira kwa vijana kupitia mpira wa miguu.

Kwa kutambua hilo, tunajua Serikali ya Tanzania haikubaki mpweke baada ya Dk. Magufuli kuiaga dunia, kwani ipo katika mikono salama na imara kabisa chini ya Rais Samia Suluhu, ambaye ni mdau mkubwa wa michezo nchini.

Hivyo, tunatarajia kuona Serikali ya Rais Samia ikitoa kipaumbele katika kuendeleza yale yote mazuri yalioachwa na Dk. Magufuli katika sekta ya michezo hususan kuboresha, kumalizia na kujenga miundombinu mipya ya viwanja, akianza kwa kuhakikisha Uwanja wa Magufuli pale Chato na ule wa Dodoma vinakamilika kwa wakati na ubora uleule kama ambavyo ilitarajiwa na mtangulizi wake.

Matarajio yetu ni kuona kila kona nchini miundombinu ya michezo hususan viwanja, vikiongezeka tena kwa ubora wakuwezesha mechi za kimataifa kuchezwa, kwani kwa kufanya hivyo kutavutia wawekezaji wengi wa soka ndani na nje ya nchi, hivyo kuongeza ajira kwa vijana.

Ni wazi kabisa, licha ya Chato kutokuwa na timu ya Ligi Kuu, lakini kuwapo kwa uwanja bora wa kisasa wilayani hapo, kutaamsha ari kwa timu za wilayani hapo kujituma zaidi, lakini pia baadhi ya timu za Ligi Kuu zinaweza kwenda kuutumia kama uwanja wa nyumbani kama ambavyo Tanzania Prisons ya Mbeya ilivyohamia Uwanja wa Nelson Mandela uliopo Sumbawanga mkoani Rukwa, hivyo hatutarajii kuona uwanja huo ukitelekezwa na kuwa gofu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Stars kutofuzu AFCON mengi yamechangia

**HIVI** sasa kila mmoja anazungumza lake juu ya timu ya Taifa ya Tanzania kushindwa kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON). Ni michuano inayotarajiwa kuchezwa Januari hadi Februari mwakani nchini Cameroon.

Alhamisi iliyopita, Taifa Stars ilizima ndoto za kutaka kucheza fainali hizo kwa mara ya pili mfululizo baada ya kuchapwa mabao 1-0 dhidi ya Equatorial Guinea ikiwa ugenini.

Tanzania ilifuzu kucheza michuano hiyo mwaka 2019 ilipocheza fainali hizo nchini Misri baada ya miaka 40.

Kwenye Kundi la J, Stars ilikuwa pamoja na Tunisia na Equatorial Guinea ambazo zimefuzu huku yenyewe na Libya ndoto zao zikiyeyuka. Hata hivyo kushindwa kufuzu AFCON kwa Stars kumepokelea kwa hisia tofauti na mashabiki wa soka nchini.

Lakini baadhi yao wanaonekana kushangaza kwa kile ambacho wao wanaona kimesababisha Stars ishindwe kusonga mbele. Kuna wanaosema uchaguzi wa wachezaji wa timu ya taifa haukuwa mzuri.

Pia wapo wanaodai kuna baadhi ya wachezaji ambao wana uwezo wa kuichezea timu ya taifa hawakuitwa na badala yake wakachukuliwa baadhi ya wachezaji ambao uwezo wao ni wa kawaida tu, au unaotia shaka.

Wengine wanadai kuwa mfumo uliotumika kwenye mechi hiyo haukuwa rafiki kwa wachezaji. Mashabiki wengine wamewatuhumu nahodha Mbwana Samatta na mwenzake Simon Msuva ambao ndiyo tegemeo kwenye kikosi cha Taifa Stars kuwa hawakuwa kwenye viwango vya bora vilivyozoeleka, wakieleza walicheza chini ya kiwango.

Watanzania wengine wanadai hakukuwa na muunganiko baina ya viungo washambuliaji na washambuliaji. Ilijaza viungo wakabaji wengi, Mzamiri Yassin, Jonas Mkude na Feisal Salum, wote wakiwa na tabia ya kukaba, na hakuna yeyote aliyekuwa anawalisha washambuliaji.

Wapo walioenda mbali zaidi na kudai eti Stars imefungwa kwa sababu tu ilijaza wachezaji wengi wa klabu ya Simba. Ili mradi tu kila mmoja anasema lake. Lakini ukweli unabaki pale pale tu, Taifa Stars haina hati miliki ya kucheza Fainali za AFCON.

Kuna nchi au mataifa makubwa ambayo yako juu kimpira, lakini yameshindwa kutinga fainali hizo, achilia mbali Tanzania. Timu ya taifa, ina matatizo mengi mno ya msingi na wala hakuna hata moja kati ya hilo ambalo mashabiki wamekuwa wakidai.

Ni maoni yao na mawazo yao, lazima yaheshimiwe, lakini ukirudi nyuma ni kwamba Watanzania tuna matatizo ya msingi kwenye soka letu, lakini tumekuwa na tabia ya kulaumu tunakoangukia tu.

Kuna nchi ambazo zimetuzidi soka na hata viwango zimeshindwa kufuzu kama DR Congo, Angola, Togo na hata Zambia, zote hizi zimeambulia patupu. Cha kusangaza nchi kama Comoro ambayo ilikuwa inafungwa mabao mpaka 15-0 na Tanzania miaka ya 1990, imefuzu AFCON.

Tatizo letu kubwa ni kwamba hatuna mipango mizuri ya uzalishaji vijana, pamoja na mafuzo ya uhakika kwa wachezaji wadogo tangu awali. Ndiyo maana wachezaji wa Kitanzania ili uwaone wanacheza vizuri ni lazima wawe wamezungukwa na nyota wa kigeni. Wakibaki wenyewe ndicho hicho kinachoonekana.

Matatizo mengine yapo nje kabisa ya uwezo wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), na hata benchi la ufundi.

Nchi kama Equtorial Guinea ilikuwa na wachezaji wengi wanaocheza ligi mbalimbali Hispania na wenye uraia wa nchi mbili, Hispania na Equatorial Guinea.

Hata Comoro imekuwa juu kwa sasa kwa sababu wachezaji wao wengi ni raia wa Comoro na Ufaransa, wakicheza ligi mbalimbali za huko.

Watanzania tuna wachezaji wengi nchi za nje ambao wazazi wao wamezaliwa Bongo, kina Yusuph Poulsen wa Denmark na wengine wengi wanaotaka kuichezea Stars, lakini wanatatizwa tu na kutokuwapo kwa uraia wa nchi mbili.

Nchi nyingi za Afrika kwa sasa wanatumia hilo ili kuwapata wachezaji wenye asili yao waliopo nje na wamekuwa wakizisaidia sana.

Tanzania tusipobadilika na kufanya hivyo, angalau kwa wanamichezo tu, basi tutaendelea kushikana uchawi, kufukuza makocha, kutiana vidole vya macho na kusutana, huku ukweli tukiwa tumeuweka mfukoni.

# Wachimbaji almasi wamshukuru Magufuli masoko ya madini

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WACHIMBAJI wadogo wa madini ya almasi katika mji wa Maganzo wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, wamemshukuru Hayati Rais John Magufuli kwa kuithamini sekta hiyo, na kuanzisha masoko ya madini.

Mbali na kuanzisha masoko hayo ya madini, pia wamemshukuru kwa kuwatambua wachimbaji wadogo wa madini, na hata kuwatengea maeneo ya uchimbaji na kutobuguziwa tena na matajiri, ambao walikuwa wakihodhi maeneo yenye madini ambayo huyaibua wao.

Wachimbaji hao walibainisha hayo juzi wakati wakizungumza na waandishi wa habari, ambao walitembelea kwenye maeneo hayo ya wachimbaji wadogo kuzungumza nao namna wanavyo muenzi Hayati Rais John Magufuli, ambaye alifariki Machi 17, mwaka huu na kuzikwa Ijumaa huko wilayani Chato mkoani Geita.

Mmoja wa wachimbaji hao, Masanja Joseph, alisema hawatamsahau Hayati Magufuli kwa mchango wake katika sekta ya madini tangu alipoingia madarakani mwaka 2015, ambapo aliwapigania pamoja na kufungua masoko ya madini.

"Sisi wachimbaji wadogo wa madini ya almasi hapa Maganzo tulikuwa tuna nyanyasika sana miaka ya nyumba kutoka kwa matajiri, lakini alipoingia tu madarakani Hayati Magufuli tukapata mtetezi wetu na kuacha kunyanyasika tena," alisema Joseph. "Zamani tulipokuwa tukipata madini, matajiri walikuwa wakitunyonya sana kwa kununua bei ambayo wanaitaka wao, lakini baada ya Hayati Rais John Magufuli kuanzisha masoko ya madini, tumekuwa tukiuza kwa bei kubwa na kupata pesa nyingi na kufanya maendeleo," aliongeza.

Naye mchimbaji wa almasi Ester Luhende, alisema kabla ya kuanzishwa masoko hayo ya madini, walikuwa hawalipi hata kodi serikalini, lakini kwa sasa wakienda kuyauza wanalipa kodi hapo hapo na kuchangia maendeleo kwenye nchi yao. Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kijiji cha Maganzo wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, Charles Manyeye, alimwomba Rais Samia Suluhu Hassan, kuendelea kuisimamia vyema sekta hiyo ya madini kama ilivyokuwa kwa Hayati Magufuli, ikiwa ina mchango mkubwa kuongeza pato la Taifa.

Aidha, alimwomba Rais Samia kuendelea kuwasimamia wachimbaji wadogo kwa kuwatetea, ili wasibuguziwe na matajiri kwa kuondolewa kwenye maeneo yao ya uchimbaji, ambayo walipewa na Hayati Magufuli, jambo ambalo litasaidia pia kuendelea kudumisha amani ya nchi.

# Wenyeviti waonywa fedha za mihuri

**Na Neema Sawaka,** MSALALA

WENYEVITI wa vijiji na vitongoji Kata ya Lunguya Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameshauriwa kutopokea fedha na kupiga mihuri ya makubaliano kati ya muuzaji na mnunuaji kwenye kipande cha ardhi kwa kuwa inaweza kuwaletea matatizo badaye ikiwamo ukwepaji wa kodi.

Hayo yalisemwa jana na mwezeshaji kutoka kituo cha msaada wa kisheria mkoani Shinyanga (Paceshi), John Shija, wakati akitoa elimu juu ya baadhi ya sheria na mpango kazi kwa wenyeviti wa vijiji, vituo vya taarifa na maarifa vilivyojengewa uwezo na mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) pamoja na wasaidizi wa msaada wa kisheria katika kata hiyo.

Shija alisema wenyeviti wengi wamekuwa wakijiingiza kwenye migogoro bila wao kujua ikiwa ni kinyume cha sheria kwani wao ndiyo wamekuwa mstari wa mbele kupiga mihuri makubaliano ya uuzaji wa kipande cha ardhi na kupokea fedha kwani wanachotakiwa ni kuthibitisha tu katika barua zao.

"Muuzaji na mnunuaji wa kipande cha ardhi wanatakiwa wasimamiwe na mwanasheria katika makubaliano yao na fedha zipokelewe na mwanasheria huyo nakulipa kodi kwani wanachokifanya siku zote kwa mazoea ni kupiga muhuri makubaliano kinyume cha sheria na kupokea fedha bila kujali inatakiwa kulipa kodi kupitia fedha hiyo," alisema Shija.

Shija alisema wengi kama ikitokea tatizo au changamoto wanaweza kujikuta kwenye hatia, hivyo aliwashauri wazingatie sheria na kuzijua kiundani wao sio sehemu ya makubaliano wala kupokea fedha bali ni wathibitishaji tu.

# Vituo vyaja kufundisha ufugaji samaki

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKALI inakusudia kuanzisha vituo vya ukuzaji viumbe maji katika halmashauri za wilaya 80 ambavyo vitatumika kama shamba darasa kwa ajili ya kufundisha wananchi namna ya kufuga samaki.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, mjini Morogoro mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilipotembelea kituo cha ukuzaji viumbe maji kinachozalisha vifaranga vya samaki cha Kingolwira, Manispaa ya Morogoro.

Ndaki alisema katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22, wizara hiyo imelenga kuanzisha vituo hivyo kwenye halmashauri ili kuongeza uzalishaji wa mabwawa ya samaki, hatua ambayo pia itaweza kusaidia kupunguvu uvuvi haramu kwenye maeneo hayo.

Alisema lengo lingine ni kuhakikisha kila halmashauri inakuwa na kituo hicho ambacho kitatumika kama shamba darasa kwa ajili ya kufundisha wananchi namna ya kufuga samaki.

Waziri Ndaki alisema mkakati wa serikali kupitia vituo hivyo vitakavyokuwapo katika halmashauri zote za wilaya ni kuwa na samaki wengi wafugwao kwa njia mbalimbali ikiwamo ya mabwawa na kufikia uzalishaji wa samaki wa asilimia 50 kwa njia ya kufuga na asilimia 50 wanaotokana na maji ya asili.

"Ili kufikia lengo la tasnia hii ya ukuzaji viumbe maji tunataka kuweka nguvu kubwa ili tuweze kuvuna rasilimali ya uvuvi iweze kusaidia lishe, ajira na kuondoa umaskini kwa wananchi," alisema Ndaki.

Alisema hivi sasa wizara hiyo imejipanga kupitia mikakati ya kuhakikisha inafikia malengo yake kupitia tasnia sambamba na mpango wa kuhakikisha inavipa uwezo mkubwa na kuvikarabati vituo vyote vya ukuzaji viumbe maji vilivyopo nchini ili kwenda sawa na uzalishaji wa vifaranga vya samaki kulingana na mahitaji yake. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Dk. Christine Ishengoma, alipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuweka jitihada mbalimbali za kuhakikisha inazalisha kwa wingi vifaranga vya samaki na kutoa elimu juu ya ufugaji wa samaki.

Alisema kamati hiyo itaangalia vyema bajeti ya wizara itakayowasilishwa kwa ajili ya mwaka wa fedha 2021/22 ili iweze kuwa na tija na kuleta matokeo chanya hususan katika tasnia ya ufugaji samaki kwa kuwa bado ni eneo jipya ambalo watu wengi wanahitaji kujifunza na kujiingiza katika ufugaji huo.

Naye Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Imani Kapinga, alisema kituo cha ukuzaji viumbe maji Kingolwira katika kutekeleza majukumu yake kati ya mwaka 2010 hadi 2020 kimetoa mafunzo kwa wananchi 11,280 kutoka mikoa mbalimbali.

Alisema pia kimezalisha vifaranga vya samaki aina ya sato zaidi ya milioni sita vilivyosambazwa maeneo mbalimbali. Baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo kwa nyakati tofauti waliipongeza Wizara hiyo kwa kuhakikisha inakiboresha kituo cha Kingolwira kwa kufanya upanuzi wa baadhi ya majengo kwa ajili ya ukuzaji viumbe maji kwa ajili ya manufaa ya wananchi.


absa

Congratulations and wishing you all the best

H.E. Samia Suluhu Hassan

The board and the entire staff of Absa Bank Tanzania Limited, wish to convey our heartfelt congratulations to the President of the United Republic of Tanzania.



# Waomba serikali itoe elimu ya mirathi

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

WAKAZI wa Kata ya Didia, Halmashauri ya Shinyanga Vijijini mkoani hapa, wameiomba serikali kutoa elimu ya mirathi katika jamii hasa kwa wananchi wanaoishi pembezoni ili kupunguza vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto vinavyojitokea mmiliki wa mali anapofariki dunia.

Retisia Shaah, mkazi wa kata hiyo aliyasema hayo jana wakati akizungumza na vyombo vya habari vinavyotekeleza mradi wa nafasi ya vyombo vya habari katika kumaliza ukatili dhidi ya wanawake na watoto unaotekelezwa na SPC kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania (WFT).

Alisema, matukio ya namna hiyo kwa baadhi ya makabila hasa kwa jamii ya kisukuma yameota mizizi na kuamini kuwa mwanamke hana haki ya kumiliki mali za marehemu na kusababisha kuongezeka kwa watoto mitaani baada ya kukosa matunzo ya familia.


Alidai kuwa yeye alikuwa ameolewa na alimkuta mwanaume katika nyumba ya kupanga, walipambana na kujenga nyumba mbili, lakini alishindwa kuendelea naye baada ya kuanza kuleta wanawake wengine ndani hasa anapokuwa safarini kwenye shughuli za kujiingizia kipato.

"Tulijenga nyumba mbili moja tulikuwa tunaishi na nyingine tumepangisha, ila mwanaume alikuwa analeta wanawake ndani na kunitaka mimi kulala chumba kingine...Nimemshtaki mara kadhaa na kumtaka tugawane mali ila yeye hataki mpaka sasa nimemwachia mali zote," alisema Shaah.

Ferister John, kwa upande wake alisema, asilimia kubwa ya kinamama na watoto wanadhulumiwa mali za waume zao na ndugu wa mwanaume na wanapojaribu kuingilia kati na kugombania mali wanaambulia kipigo au kutishiwa kutengwa na familia wanapojaribu kwenda kuwashtaki.

Shukrani Peter, alisema baba na mama wanapokuwa na mali ikatokea mmoja wapo amefariki, ndugu wanajitokeza na kugombania mali hasa mashamba na mara nyingi vitendo hivyo wanafanyia watoto ambao hawajui chochote na mwisho wa siku wanaanza kuhangaika mitaani.

Kwa upande wake Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Jackson Maganga, alisema matukio ya namna hiyo yameota mizizi kwa baadhi ya makabila kuamini mwanamke hana haki ya kumiliki mali au ardhi na kutoa maamuzi ndani ya familia baada ya mwanaume kufariki.



Mkazi wa jijini Dar es Salaam, Masuma Bharwani, akitia saini kitabu cha maombolezo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli, katika Ofisi za Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kasi ya upatikanaji maji Lindi yapaa

**Na Said Hamdani,** LINDI

IDADI ya wananchi wanaopata na kutumia huduma ya majisafi na salama kwa matumizi mkoani Lindi, imeendelea kuongezeka kutoka asilimia 42.9 hadi kufikia 61.5, baada ya serikali kuupatia mkoa huo fedha za utekelezaji wa miradi kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Kaimu Mkuu wa Mkoa huo, Shaibu Ndemanga, aliyaeleza hayo kwenye Ibada maalumu ya kumwombea aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, iliyofanyika uwanja wa Ilulu mjini Lindi.

Ndemanga aliyaeleza hayo alipokuwa anaelezea utekelezaji wa miradi ya maendeleo mkoani humo, tangu kiongozi huyo alipoingia madarakani mwaka 2015 hadi 2021, ambapo kwa kipindi cha uongozi wake mkoa ulishapelekewa jumla ya Sh.72,420,745,291 kutekeleza miradi ya huduma ya maji.

Alisema kutokana na utekelezaji wake huo, idadi ya wananchi wanaopata huduma ya maji na salama kwa mijini sasa, imeongezeka hadi kufikia asilimia 71.

Ndemanga ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Lindi, alisema mafanikio hayo yametokana na Serikali ya Hayati Magufuli, kutekeleza miradi ya ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya maji mijini na vijijini chini ya usimamizi wa Wakala wa Maji Mkoa (LUWASA).

Ilieleza katika kuhakikisha wananchi wanaoathiriwa na tatizo la upatikanaji wa majisafi na salama kila Halmashauri ya Mkoa wa Lindi, zimepatiwa mgao wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wake, ambapo Ruangwa imepewa Sh. 8,647,406,808 kutekeleza miradi mikubwa ya Kitandi na Ruangwa mjini.

Kilwa imepatiwa Sh. 260,775,860 kutekeleza miradi ya maji Kata ya Mingumbi na Masoko, huku Sh. 3,173,582,199 zikipelekwa Nachingwea kwa ajili ya upanuzi wa mradi wa maji kutokea Ngwinji, Wilaya ya Masasi, Mkoa wa Mtwara hadi Nachingwea. Sh. 2,723,864,420 zimepelekwa Liwale kutekeleza miradi iliyopo vijiji vya Kichonda, Mikunya, Mbaya na Mtumbwa.

Ndemanga LUWASA imepewa Sh. 41,117, 849,038 wakati Manispaa ya Lindi, imepatiwa Sh. 7,588,760, 308 kutekeleza mradi wa Nandambi, Chikonji na Kineng'ene na Sh. 1,908, 506,658 zimepelekwa Halmashauri ya Mtama kwa mradi wa Nyangamara, ukarabati wa mradi Kijiji cha Namunda, Ruhokwe na Mnolela.

Akizungumza na wananchi waliojitokeza kwenye ibada hiyo, Ndemanga alisema njia pekee ya kumuenzi kiongozi huyo, ni wananchi kuongeza kasi ya uwajibikaji katika uzalishaji mali viwandani na mashambani.

"Hakuna njia nyingine ya kumuenzi mpendwa wetu huyu, bali ni kuongeza jitihada katika kufanyakazi," alisema.

Viongozi wa dini, akiwamo Askofu wa Jimbo Katoliki la Lindi, Mhashamu Bruno Ngonyani, mchungaji Baraza la Makanisa ya Pentecost, Dismas Rogers, mchungaji Kanisa la CCCT na Jimbo la Kikristo Tanzania, Wayuziman Simungu na mwakilishi wa BAKWATA Mkoa wa Lindi, Yusufu Amani, walisema watamkumbuka Hayati Dk. Magufuli kwa mambo mengi mazuri.

# Mil. 789/- kutengeneza barabara za Songea

**Na Stevie Chindiye,** SONGEA

WAKALA wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma, imeidhinishiwa Sh. milioni 789 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya matengenezo ya barabara kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Hayo yalisemwa na Meneja wa TARURA katika halmashauri hiyo, Mhandisi John Ambrosi, kwamba halmashauri hiyo ina mtandao wa barabara zenye urefu wa kilometa 1,057, kati ya hizo, barabara za lami ni kilometa 13.77, kilometa 250 ni barabara za changarawe na barabara za udongo ni zaidi ya kilometa 700.

Alisema katika mwaka wa fedha 2020/2021 TARURA inatekeleza mikataba sita ya ujenzi yenye thamani ya shilingi bilioni 1.396, kati ya hizo shilingi milioni 701 ni kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Muhukuru na fedha inayobakia ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara, alisema. Hata hivyo, alisema katika mwaka wa fedha wa 2019/2020 TARURA ilikuwa na mradi wa ujenzi wa daraja la Muhukuru ambao unatekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Alisema utekelezaji wa miradi hiyo ulianza Agosti 2020, na kwamba hadi kufikia Novemba 2020 jumla ya miradi minne kati ya sita ilikuwa imetekelezwa ambapo hadi kufikia Juni mwaka huu miradi yote inatarajiwa kukamilika kwa asilimia 100.

Hata hivyo, alisema licha ya jitihada zinazofanywa na TARURA kuimarisha barabara, madaraja na vivuko, kumekuwa na changamoto mbalimbali zinazoathiri miundombinu zikiwamo magari yenye uzito mkubwa na mvua za masika zinazoanza Novemba hadi Aprili kila mwaka.

Baadhi ya wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea katika Kijiji cha Litowa waliishukuru TARURA kwa kuwasaidia kukarabati kivuko kinachounganisha kitongoji cha Goliama na Litowa.

Christina Njovu na Egno Mwalongo walisema kivuko hicho kimekuwa kero kwao kwa sababu magari hayawezi kuvuka pia kinahatarisha usalama wao hivyo wanaiomba serikali kuwajengea daraja la kudumu.

Mhandisi Ambrosi alisema wanatambua changamoto hiyo ambapo hivi sasa hawajapata fedha za kujenga daraja la kudumu.

Amesema TARURA imejenga kivuko cha mbao chenye urefu wa kilometa 21 na kwamba wamekuwa wanakifanyia matengenezo ya mara kwa mara wakati serikali inatafuta fedha za kujenga daraja la kudumu ili kumaliza kero hiyo kwa wananchi.

HABARI KITAIFA

# Kinamama waomba kupatiwa elimu ya umiliki wa mirathi

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

WAKAZI wa Kata ya Didia, Halmashauri ya Shinyanga Vijijini mkoani hapa, wameiomba serikali kutoa elimu ya mirathi katika jamii hasa kwa wananchi wanaoishi pembezoni.

Lengo ni kupunguza vitendo vya kikatili kwa wanawake na watoto wadogo vinavyojitokeza pale mmiliki wa mali anapofariki dunia.

Retisia Shaah, mkazi wa kata hiyo aliyabainisha hayo wakati akizungumza na vyombo vya habari vinavyotekeleza mradi wa nafasi ya vyombo vya habari katika kumaliza ukatili dhidi ya wanawake na watoto unaotekelezwa na SPC kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania (WFT).

Alisema matukio ya namna hiyo kwa baadhi ya makabila yameshamiri na yanaamini kuwa mwanamke hana haki ya kumiliki mali za marehemu na kusababisha kuongezeka kwa watoto wadogo mitaani baada ya kukosa matunzo ya familia.

Aidha, alidai kuwa yeye alikuwa ameolewa na mwanaume na alimkuta katika nyumba ya kupanga, walipambana na kujenga nyumba mbili, lakini alishindwa kuendelea nae baada ya kuanza kuleta wanawake wengine ndani, hasa anapokuwa safarini kwenye shughuli za kujiingizia kipato.

"Tulijenga nyumba mbili moja tulikuwa tunaishi na nyingine tumepangisha, ila mwanaume alikuwa analeta wanawake ndani na kunitaka mimi kulala chumba kingine ...nimemshtaki mara kadhaa na kumtaka tugawane mali ila yeye hataki mpaka sasa nimemwachia mali zote," alisema Shaah.

Pia Ferister John, alisema asilimia kubwa ya kinamama na watoto wamekuwa wakidhulumiwa mali za waume zao na wanandugu wa mwanaume, na wanapojaribu kuingilia kati na kugombania mali wanaambulia kipigo au kutishiwa kutengwa na familia wanapojaribu kwenda kushtaki.

Shukrani Peter alisema baba na mama wanapokuwa na mali ikatokea mmoja wapo amefariki, ndugu wanajitokeza na kugombania mali hasa mashamba na mara nyingi vitendo hivyo wanafanyia watoto wadogo, ambao hawajui chochote na mwisho wa siku wanaanza kuhangaika mitaani.

Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Jackson Maganga, alisema matukio ya namna hiyo yameota mizizi kwa baadhi ya makabila yanaamini mwanamke hana haki ya kumiliki mali au ardhi na kutoa maamuzi ndani ya familia, baada ya mumewe kufariki dunia.

Alisema migogoro ya kifamilia ndio inayoathiri watoto wadogo kisaikolojia kwa kiasi kikubwa kwa sababu inasababisha watoto kukosa haki zao za kimsingi, ikiwamo elimu, chakula na mavazi kwa wazazi kuendekeza ugomvi wa ugawaji wa mali za marehemu.

# Jela miaka 9 kutorosha, kubaka mtoto

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MAHAKAMA ya Mkoa Wete imemhukumu Mohamed Khamis Ali (25) mkaazi wa Utaani Wete, kifungo cha miaka tisa jela na kulipa fidia ya Sh. 1,500,000 baada ya kupatikana na kosa la kutorosha na kubaka.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Abdalla Yahya Shamhun, baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili, na kujiridhisha bila kuacha shaka yoyote kuwa mshtakiwa alitenda makosa.

Alisema mahakama ilithibitisha kosa hilo pasi na kuwa na chembe ya shaka juu ya ushahidi uliotolewa, hivyo mshtakiwa atalazimika kwenda jela kwa miaka tisa na kumlipa fidia mwathirika, ambaye kwa sasa ni marehemu, shilingi 1,500,000.

Kabla ya kusomewa hukumu hiyo, Mwendesha Mashtaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba, Ali Amour Makame, aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa ili iwe fundisho kwake na kwa wengine wenye tabia kama yake.

Naye mshtakiwa alipopewa nafasi ya kusema, aliiomba mahakama impunguzie adhabu kwani ni kosa lake la kwanza na ana familia na watoto ambao wanamtegemea.

Mshtakiwa huyo alitenda makosa mawili, ambapo la kwanza alilitenda siku na tarehe isiyojulikana saa 2:00 usiku katika Shehia ya Utaani Wilaya ya Wete, kwa kumtorosha mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 15 bila ridhaa a wazazi wake kutoka nyumbani kwao na kwenda nae kwenye nyumba yake. Kosa la pili ni kumbaka mtoto huyo.

Kufanya hivyo ni kosa kisheria kinyume na vifungu cha 108 (1), (2), (e) na 109 (1) vya Sheria Nambari 6 ya mwaka 2018 Sheria ya Zanzibar.



Mwendesha pikipiki akisafirisha mihogo kuipeleka sokoni Mkuranga, mkoani Pwani juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Katavi, Lindi zashauriwa mikakati uzalishaji asali

**Na Said Hamdani,** LINDI

SERIKALI imewataka watendaji mikoa ya Lindi na Katavi, kuhakikisha inakuwa na mikakati mahususi itakayoiwezesha jamii kupata elimu ya ufugaji nyuki, itakayowasaidia kuongeza uzalishaji asali.

Asali hiyo utaimarisha lishe na kipato kwa lengo la kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini. Wito huo ulitolewa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, wakati anazindua mashine ya kuchakata magogo kwa wadau wa misitu vijiji 18 vilivyopo wilaya za Ruangwa na Nachingwea, mkoani Lindi.

Akizindua mashine hiyo aina ya merold yenye thamani ya Sh. milioni 110 kutoka Finland katika Kijiji cha Narung'ombe, Wilaya ya Ruangwa, Waziri Ndumbaro amewataka wadau hao kuhakikisha wanaitumia mashine hiyo kwa uangalifu iweze kuwasaidia kuzalisha kwa wingi magogo na mbao.

Alisema Mkoa wa Lindi ni wa pili nchini, kwa kuwa misitu mikubwa ukiongozwa na Katavi, huku akizitaka halmashauri kutumia fursa hiyo, kuwa na mikakati itakayowawezesha wananchi kupata elimu inayohusiana na ufugaji wa nyuki kwa ajili ya asali. Alisema licha ya Lindi kushika nafasi ya pili kwa kuwa na misitu mikubwa, bado zao la asali inayovunwa na Watanzania inatoka mkoa mmoja tu wa Tabora.

Dk. Ndumbaro alisema serikali inatambua na kuzipa umuhimu rasilimali zilizopo katika Mkoa wa Lindi, kwani upo mpango mahsusi katika kuboresha miundombinu yake kwa kuzitangaza ndani na nje.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Shaibu Ndemanga, alisema uzinduzi wa mashine hiyo itasaidia kuongeza thamani ya mazao ya misitu katika vijiji husika sambamba na kuhamasisha jamii usimamizi endelevu wa misitu na kuwaletea tija na kuwainua kiuchumi.



Wasamaria wema wakisaidiana na askari wa usalama barabarani kusukuma daladala lililokuwa limezimika katikati ya barabara eneo Tangi Bovu, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kanisa lataka kudumishwa mshikamano

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

KANISA la Neema ya Kikristo la Msamvu, Manispaa ya Morogoro, limewataka Watanzania pamoja na waumini wa kanisa hilo kudumisha na kuendeleza mshikamano pamoja na upendo kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dk. John Magufuli, ili kumpanga nguvu Rais Samia Suluhu Hassan kuendeleza yote yalipangwa katika kipindi hiki.

Mchungaji wa Kanisa hilo, Condrad Conwel, alitoa rai hiyo wakati akizungumzia namna kanisa hilo lilivyoguswa na kifo cha Hayati Dk. Magufuli kilichotokea Machi 17, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Alisema katika maisha ya uongozi wa Hayati Dk. Magufuli alikuwa ni mtu mwenye kuonyesha upendo kwa wananchi wake na kuhimiza mshikamano kwenye jamii, huku akiwa ni mtetezi wa wanyonge. "Nawaomba Watanzania wenzangu katika kipindi hiki kinahitajika kuombea nchi yetu iendelee kuwa na amani na kunahitajika kuwapo mshikamano wa hali ya juu ili kumpa nguvu Rais wetu Mama Samia kuendeleza yale yote yaliyokusudiwa kufanywa na Hayati Dk. Magufuli," alisema Mchungaji Conwel.

Mchungaji Conwel alisema katika kipindi hiki pia Watanzania wanapaswa kumwombea dua njema Rais Samia ikiwa na kumuunga mkono ili aweze kuwaongoza Watanzania.

Conwel pia kupitia waumini wa kanisa hilo alimwomba Rais Samia kuendeleza mema yote aliyofanywa na mtangulizi wake, ambaye sasa amepumzika katika nyumba yake ya milele.

Nao baadhi ya waumini wa kanisa hilo kwa nyakati tofauti walieleza kuwa Hayati Dk. Magufuli atakumbukwa kutokana na kuwa chachu ya mabadiliko ya kimaendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Walimtaja kuwa ni kiongozi ambaye aliweka vipaumbele kwenye huduma za kijamii kama uboreshaji wa afya, elimu hususani mfumo wa elimu bila malipo kwa wanafunzi, miundombinu na uimarishaji wa uwajibikaji kwa watumishi wa umma na kupambana na wala rushwa.

# Mwanafunzi mwenye ulemavu akumbukwa

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MWANAFUNZI wa darasa la tano Shule ya Msingi Masasi katika Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara ambaye ni mwenye ulemavu wa viungo, Mwanaalusi Issa, amepatiwa msaada wa baiskeli yenye thamani ya Sh. 475,000 ili imsaidie kuondokana na kutembea kwa kutumia mikono na magoti.

Msaada huo ulitolewa na Shirika lisilo la kiserikali la Kalamu Education Foundation kutoka Dar es Salaam, ambalo linajihusisha na kusaidia jamii hasa makundi maalumu.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, Mratibu wa shirika hilo tawi la Masasi, Hussein Mchomolo, alisema wameamua kumsaidia mwanafunzi huyo baada ya kuguswa na kikwazo kinachomkabili cha ukosefu nyenzo hiyo.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Ituyani Chikomo, alilipongeza shirika kwa kutoa msaada huo na kuiomba jamii kujenga utamaduni wa kutoa misaada kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ikiwamo baiskeli pamoja na mafuta ya ngozi kwa ajili wenye ualbino.

# Yatima kituo ca Umra Dar: Samia ni chaguo la Mungu

**Na Jumanne Juma**

WATOTO yatima wanaolelewa katika Kituo cha Umra jijini Dar es Salaam, wamefanya dua maalum ya kumwombea aliyekuwa Rais, Hayati Dk. John Magufuli na kumwelezea mrithi wake, Rais Samia Suluhu Hassan, kuwa ni chaguo la Mungu.

Walifanya dua hiyo katika kituo hicho kilichopo Magomeni juzi, iliyokwenda sambamba na upokeaji wa misaada mbalimbali kutoka kampuni ya Luckwell ya China. Misaada hiyo ililenga kuwafariji watoto hao katika kipindi cha maombolezo.

Akiongoza dua hiyo, Mwasisi wa Vituo vya Umra, Rahma Juma, alisema siku ambayo Rais Samia alikula kiapo ndiyo siku aliyokata mbeleko ya kuwabeba Watanzania hususan wanyonge na yatima.

"Cheo hicho kachaguliwa na Mungu. Hakuchaguliwa na mtu, huwezi kumchagua mtu kabla Mungu hajamchagua," alisema Rahma.

Mtoto Abdulhakim Mohammed, alisema wanamwombea Rais Samia Mungu ampe nguvu ya kufanyaa kazi kama ilivyo kuwa kwa Hayati Rais Dk. Magufuli.

"Tunaimani Rais Samia atatusaidia, hivyo tunamwomba Mungu amwondolee balaa, maradhi ya kila aina na atukumbuke yatima," alisema.

Mtoto Yasira Dauda, alisema Samia kuongoza taifa ni siri ya Mwenyezi Mungu. "Tunaomba asichoke kutubeba," alieleza mtoto huyo.

Akikabidhi misaada kwa watoto hao, Meneja wa Kampuni ya Lucky, Well Feng Hun Chen, ambaye ni raia wa China, alimwelezea Hayati Rais Dk. Magufuli kuwa aligusa maisha ya wanyonge wakiwamo watoto, na kwamba ili kumuenzi, ni wajibu wa jamii kutoa kwa ajili ya makundi yenye mahitaji maalumu.

"Tumekabidhi msaada huu wakati wa siku ya maziko ya Hayati Dk. Magufuli ili kuwafariji yatima kwa sababu marehemu aliwathamini na kuwajali watu wenye mahitaji maalumu kama hawa," alisema Chen.

Alisema msaada huo unaohusisha mchele tani moja, sukari, mafuta ya kupikia, sabuni ya unga na miche ni kwa ajili ya watoto katika kipindi cha maombolezo na kuahidi kuwa wataendelea kusaidia jamii ili kumuenzi Hayati Dk. Magufuli.

Mfadhili wa kituo hicho cha Umra chenye watoto 117, Juma Gurumo, alisema, msiba wa Dk. Magufuli ni mkubwa, hivyo waliona kuna wajibu wa kuchangia kwa kuwapa yatima mahitaji muhimu hasa ya chakula.

"Tunaamini Hayati Rais Dk. Magufuli aliwajali wanyonge na wenye mahitaji, hivyo wakati tukiomboleza tumuenzi kwa kukumbuka kundi hili," alisema Gurumo.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 7 LIGI KUU BARA WALIOTESA KUFUZU AFCON... UK 14




# NYOTA WATANO WANAOWEZA KUUZWA JUVE MAJIRA YA JOTO

**TURIN, Italia**

JUVENTUS imetawala soka la Italia kwa muongo mmoja uliopita. Walishinda mara tisa mfululizo taji la Ligi Kuu Italia, Serie A, shukrani kwa kikosi bora.

Kwa kipindi hicho wamesajili baadhi ya wachezaji bora kabisa duniani, lakini si wote ambao wamechangia mafanikio ya klabu hiyo.

Mlipuko wa janga la virusi vya corona umeitikisa kiuchumi Juventus kwani mapato yake yamepungua kwa asilimia 20% kwa msimu wa 2020-21.

Hivyo kutokana na hilo, litaifanya klabu hiyo kupunguza mishahara au kuachana na wachezaji wenye mishahara mikubwa kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Makala haya yanaangalia wachezaji watano ambao wanaweza kuuzwa na Juventus kipindi cha majira ya joto, shuka nayo sasa...

**#5. Merih Demiral**

Juventus mara zote imekuwa na safu imara ya ulinzi. Huku beki mkongwe, Giorgio Chiellini, akitarajiwa kustaafu hivi karibuni, 'Bianconeri' walisajili mabeki wawili msimu uliopita.

Matthijs De Ligt, ambaye alitua hapo Juventus kipindi cha majira ya joto mwaka 2019, anachukuliwa kama mmoja wa walinzi bora vijana wanaochipukia duniani na ndio mrithi wa Chiellini. Juventus wenyewe wameshaweka wazi kwamba raia huyo wa Uholanzi hawezi kuuzwa hivi karibuni. Hivyo kama wakihitaji kufumua idara yao ya ulinzi, basi Merih Demiral ndiye atakayeuzwa.

Mlinzi huyo raia wa Uturuki amekuwa akitumika mara chache chini ya kocha, Andrea Pirlo msimu huu na kwa muda huo mdogo anaopata amekuwa akionyesha kiwango cha kuvutia. Lakini amekua chaguo la nne mbele ya Leonardo Bonucci, De Ligt na Chiellini.

**#4. Alex Sandro**

Mchezaji ambaye kwa muda mrefu amekuwa akitajwa kutaka kuondoka Juventus ni mlinzi wa kushoto, Alex Sandro. Raia huyo wa Brazil ni mmoja wa wachezaji bora kwenye nafasi yake, lakini majeraha yamekuwa yakimsumbua mara kwa mara.

Kwa mujibu wa ripoti, 'Kibibi Kizee' hicho cha Turin kipo tayari kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 kwa euro milioni 25. Huku mkataba wake ukiwa unamalizika mwaka 2023, Juventus hawatakubali kumwachia aondoke bure, hivyo wanaweza kumuuza mwishoni mwa msimu huu.

**#3. Aaron Ramsey (Juventus)**

Aaron Ramsey amekuwa na wakati mgumu pale Juventus, hasa chini ya Andrea Pirlo msimu huu. Raia huyo wa Wales amecheza mechi 18 kwa msimu huu, akifunga mabao mawili na kutoa pasi za mwisho tano.

Ramsey amekuwa akihusishwa na mpango wa kutaka kurudi kwenye Ligi Kuu England, ingawa kiwango chake hakijawa bora kama alivyokuwa pale Arsenal.

Pia Bianconeri hao wanaweza kumtoa mchezaji huyo kwa kubadilishana na wachezaji wengine, kwani mkataba wake unamalizika mwaka 2023.

**#2. Paulo Dybala**

Paulo Dybala amekuwa mmoja wa wachezaji muhimu wa Juventus tangu kuwasili kwake akitokea Palermo. Katika miaka ya hivi karibuni kiwango cha Dybala kimeshuka sana.

Hakuna shaka yoyote juu ya kipaji chake, lakini Dybala ameshindwa kuonyesha ubora wake kwa kipindi cha msimu huu chini ya Pirlo na ameshindwa kuwa patina mzuri wa Cristiano Ronaldo.

Na ripoti zinasema kwamba, Chelsea na Tottenham Hotspur zina nia ya kutaka kumsajili mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Argentina ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu. 'Bianconeri' bado hawajafikia makubaliano ya kuongeza mkataba mpya na Dybala.

Na inaeleweka kwamba, Dybala anataka kulipwa mshahara mkubwa kitu ambacho Juventus hawatakuwa tayari kukifanya. Kutokana na hilo, kuna uwezekano mkubwa akauzwa mwishoni mwa msimu huu.

**#1. Cristiano Ronaldo**

Cristiano Ronaldo ni mchezaji anayependa kushinda mataji katika kila timu anayocheza. Ronaldo amekuwa na kiwango bora tangu kutua kwake Juventus kipindi cha majira ya joto mwaka 2018. Amekuwa mfungaji bora wa klabu hiyo kwa misimu miwili iliyopita. Pia msimu huu anaongoza kwenye orodha ya wafungaji.

Mkurugenzi wa Juventus, Fabio Paratici hivi karibuni alidai kwamba, klabu inaangalia uwezekano wa kumbakiza mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or na mkataba wake unamalizika mwaka 2022.

Zaidi ni kwamba, Ronaldo analipwa mara nne zaidi ya mchezaji yeyote wa Juventus. Hicho kinaweza kuwa kigezo cha Juventus kuamua kumuuza kabla ya mkataba wake kufikia mwisho.

Kama Bianconeri watashindwa kutwaa taji msimu huu, itakuwa ngumu kumbakiza mchezaji huyo. Lakini kumuuza Ronaldo kipindi hiki cha majira ya joto kutaisaidia Juventus kupata fedha za kusajili wachezaji wengine.

## ISIKUPITE

PETR Cech ndiye kipa anayeshikilia rekodi ya kucheza mechi nyingi bila kuruhusu bao 'Clean Sheets' (24) kwenye Ligi Kuu England kwa msimu mmoja, akifanya hivyo msimu wa 2004-05. Anafuatiwa na Peter Schmeichel - Clean Sheets 21 (1994-95), Edwin van der Sar - Clean Sheets 21 (2008-09), David Seaman - Clean Sheets 20 (1993-94) na Pepe Reina - Clean Sheets 20 (2005-06).



# MAGOLIKIPA 10 WANAOLIPWA MISHAHARA MIKUBWA DUNIANI

**LONDON, England**

WACHEZAJI wa mpira wa miguu ni kati ya wanamichezo wanaolipwa zaidi duniani kwa sasa. Hata hivyo, wachezaji hao wamekuwa wakilipwa tofauti, yaani mishahara ya washambuliaji na viungo imekuwa mikubwa zaidi kuliko wanaocheza nafasi nyingine.

Mabeki na magolikipa wengi wao wamejikuta wakilipwa mishahara midogo tofauti na kazi yao uwanjani.

Kocha wa zamani wa Manchester United, Sir Alex Ferguson, aliwahi kusema "golikipa ana thamani ya pointi 15 kwa msimu" na sasa klabu zinaonekana kufuata msemo huo, kwani kama ukitaka kushinda mataji unahitaji kuwa na golikipa bora kabisa.

Na matokeo yake sasa kuna magolikipa ambao wanapata mishahara mikubwa zaidi kuliko wachezaji wenzao.

Makala haya yawaangalia magolikipa 10 ambao wanalipwa mishahara mikubwa zaidi duniani kwa sasa, hawa hapa...

**#10. Wojciech Szczęny (Juventus) - Pauni 130,000 kwa wiki**

Wojciech Szczęny amekuwa na muda zaidi wa kucheza akiwa na Juventus kwa misimu mitatu, tofauti na kipindi cha miaka nane aliyokaa Arsenal kwenye Ligi Kuu England. Golikipa huyu wa Poland alijiunga na Juventus mwaka 2017 kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni 10, awali akiwa msaidizi wa Gianluigi Buffon, lakini akajikuta akichukua nafasi ya kuwa golikipa chaguo la kwanza mwaka 2018 kwa sababu Buffon alikuwa majeruhi.

Na sasa Juventus wameamua kumfanya kuwa mmoja wa makipa wanaolipwa zaidi duniani, kwani wanampa mshahara wa pauni 130,000 kwa wiki.

#9.Kasper Schmeichel (Leicester City) - Pauni 130,000 kwa wiki

Kasper Schmeichel amekuwa na Leicester City kwenye milima na mabonde tangu alipohamia hapo East Midlands akitokea Leeds United mwaka 2011, akiwa ameanza kucheza soka lake kule Manchester City.

Mchezaji huyo alikuwa kwenye kikosi cha kocha, Claudio Ranieri kilichotwaa taji la Ligi Kuu England msimu wa 2015-16 na alicheza kila dakika msimu ule huku akicheza mechi 15 bila kuruhusu bao wakati wakibeba taji hilo kwa mara ya kwanza.

Mchezaji huyo, mwaka 2018 akawa ndiye anayelipwa mshahara mkubwa zaidi kwa kupewa pauni 130,000 kwa wiki, kabla ya Jamie Vardy kuongezewa mkataba ambao sasa unamfanya alipwe pauni 140,000 kwa wiki.

**#8.Alisson Becker (Liverpool) - Pauni 150,000 kwa wiki**

Bingwa mtetezi wa Ligi Kuu England, Liverpool ni moja ya timu yenye kikosi bora kabisa duniani na golikipa Alisson alikuwa msaada mkubwa wakati vijana hao wa kocha, Jurgen Klopp walipobeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi Kuu baada ya kutua hapo Anfield mwaka 2018.

Ana rekodi ya kucheza mechi 35 bila kuruhusu bao katika michezo 70 na msimu huu majeruhi yamemweka benchi. Pamoja na yote anaweka mfukoni pauni 150,000 anazolipwa kwa wiki.

**#7. Kepa Arrizabalaga (Chelsea) - Pauni 150,000 kwa wiki**

Kuna wakati inakuwa ngumu kuamini kwamba, golikipa wa sasa wa Chelsea, Kepa Arrizabalaga anashikilia rekodi ya kuwa kipa ghali zaidi duniani. Golikipa huyo raia wa Hispania mara kwa mara amekuwa akikosa nafasi kwenye kikosi cha kwanza mbele ya Willy Caballero na Edouard Mendy.

Kepa amekuwa na rekodi mbaya kwenye Ligi Kuu England, kwani katika mechi 72, ameruhusu mabao 92 huku akicheza mechi 22 bila kuruhusu bao. Mchezaji huyo ndio kwanza ana umri wa miaka 26 na mshahara wake ni pauni 150,000 kwa wiki.

**#6. Thibaut Courtois (Real Madrid) - Pauni 150,000 kwa wiki**

Ni golikipa namba moja wa Ubelgiji na Thibaut Courtois alikuwa na msimu wa kukumbukwa 2019-20 wakati alipocheza mechi 18 bila kuruhusu bao na akafungwa mabao 20 kwenye mechi 34 za LaLiga na Real Madrid wakalibeba taji.

Mhitimu huyo wa akademi ya Genk amekuwa mmoja wa magolikipa bora duniani kwa sasa. Amefurahia mafanikio mengi akitwaa mara mbili taji la LaLiga na Ligi Kuu England na pia kung'ara kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kwa sasa analipwa pauni 150,000 kwa wiki na Los Blancos ambapo mkataba wake na Madrid unamweka hapo hadi mwaka 2024.

**#5. Manuel Neuer (Bayern Munich) - Pauni 259,000 kwa wiki**

Manuel Neuer atakumbukwa kwenye historia kama mmoja wa magolikipa bora kabisa kwenye mchezo wa soka duniani.

Msimu uliopita akiwa na Bayern Munich aliweka rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kwenye historia ya soka la Ulaya kushinda mataji matatu kwa msimu mmoja mara mbili.

Neuer mwenye umri wa miaka 35, alijiunga na Bayern kipindi cha majira ya joto mwaka 2011 na tangu hapo amechaguliwa kuwa golikipa bora duniani mara nne. Bado hajasaini mkataba mpya na mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, ambapo wa sasa unamalizika mwaka 2023 na anachukua kitita cha pauni 259,000 kwa wiki, na kumfanya kuwa mchezaji wa pili anayelipwa mshahara mkubwa zaidi nyuma ya Robert Lewandowski kwenye ligi hiyo.

**#4. Sergio Rico (Paris Saint-Germain) - Pauni 282,728 kwa wiki**

Golikipa wa Paris Saint-Germain, Sergio Rico ni kipa mwenye kipaji, kwani amethibitisha hilo wakati akiwa na Sevilla, Fulham na sasa PSG.

Golikipa huyo wa Hispania alicheza kwa mkopo kwa mara ya kwanza Fulham msimu wa 2018-19 na baadaye msimu uliopita akatua PSG akitokea Sevilla. Baada ya kuwa na kiwango cha kuvutia miamba hao wa Jiji la Paris wakaamua kumsajili kwa mkataba wa kudumu Septemba mwaka jana na atakaa hapo hadi mwaka 2024 na analipwa kiasi cha pauni 282,728 kwa wiki.

**#3. Keylor Navas (Paris Saint-Germain) - Pauni 328,330 kwa wiki**

Keylor Navas bila shaka yoyote alijiwekea rekodi ya kuwa mmoja wa magolikipa bora Ulaya wakati akicheza kule Real Madrid kwa kipindi cha miaka mitano na baadaye kuhamia Paris Saint-Germain kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Kipa huyo mwenye umri wa miaka 33, amekuwa golikipa wa kwanza wa Costa Rica kuwachezea miamba hao wa Ligi Kuu Ufaransa na katika msimu wake wa kwanza aliisaidia kutinga fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya. Amecheza mechi 71 kati ya 213 bila kuruhusu bao.

Mchezaji huyo anatajwa kama mmoja wa magolikipa bora wa wakati wote kutoka bara la Amerika Kusini na halijawa jambo la kushangaa kuona PSG wanamlipa mshahara wa pauni 328,330 kwa wiki.

**#2. Jan Oblak (Atletico Madrid) - Pauni 350,000 kwa wiki**

Jan Oblak mara moja aliwahi kutajwa kama Lionel Messi wa magolikipa na kocha wa Atletico Madrid, Diego Simeone, na raia huyo wa Slovenia amelithibitisha hilo kwenye LaLiga.

Oblak ameokoa mashuti hatari 636 kati ya 819 aliyokutana nao kwenye Ligi Kuu Hispania tangu alipohamia Madrid na hivyo kumfanya kushinda tuzo ya Zamora mara nne mfululizo kama golikipa bora wa mwaka wa LaLiga kati ya mwaka 2015 na 2019. Oblak pia anashikilia rekodi ya kucheza mechi nyingi bila kuruhusu bao, akifikisha mechi 100 kati ya 182.

Na Atletico Madrid hawakuwa na tabu kumpa mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki na pia mkataba wake una kipengele cha kuuzwa kwa pauni milioni 87.

**#1. David De Gea (Manchester United) - Pauni 375,000 kwa wiki**

David De Gea si tu ndiye golikipa anayelipwa mshahara mkubwa zaidi, lakini kwa sasa ndiye mchezaji anayelipwa mshahara mkubwa zaidi kwenye Ligi Kuu England. Raia huyo wa Hispania alisaini mkataba mpya Septemba mwaka jana hapo Man United baada ya uvumi kuzagaa kwamba anataka kuondoka kwa mabingwa hao mara 13 wa England.

Hata hivyo, katika misimu ya hivi karibuni, kiwango chake kimeshuka na Novemba mwaka huu atatimiza umri wa miaka 30, lakini bado ana nafasi kubwa ya kung'ara popote.


Kiwango chake kiliifanya Man United kuamua kumpa mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki.



DE GEA

## Nukuu

Ni wazi kwamba, [Gareth] Bale hakuwa na hana furaha kwa kipindi anachocheza Tottenahm, bahati mbaya si yeye tu, wachezaji wote hawajawa na furaha chini ya Kocha Jose Mourinho, hilo liko wazi kabisa," **Rais wa zamani wa Real Madrid, Ramon Calderon.**



"Wanamichezo wanapaswa kuwa wanamichezo na wanasiasa wanapaswa kuwa wanasiasa. Wanamichezo wanaunganisha dunia, siasa zinaigawa, jukumu letu ni kuunganisha ulimwengu kwa kufanya mambo ambayo yataunganisha jamii," **mshambuliaji wa AC Milan, Zlatan Ibrahimovic, akimkosoa nyota wa kikapu wa Marekani, LeBron James, kutokana na kujiweka mbele katika masuala ya siasa.**



"Tuna wakati mgumu, mchezo huu hautakuwa rahisi hata kidogo, na hakuna mechi rahisi, hivyo tutachukua tahadhari zote, hatuangalii sana matokeo kwenye Ligi Kuu England, maana mashindano haya ni tofauti na kila timu inaingia kwenye kila mchezo kwa ari tofauti. Liverpool wanaweza kuwa na wakati mgumu kule England, lakini wakatoa upinzani mkubwa zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, tunauchukulia **mchezo huu kwa umakini wa hali ya juu zaidi," Kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane baada ya kupangwa kukutana na Liverpool robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.**



# WACHEZAJI 7 LIGI KUU BARA WALIOTESA KUFUZU AFCON

**Na Adam Fungamwango**

PAMOJA na timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, kushinda kutinga kwenye Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) zitakazofanyika nchini Cameroon mwakani, baadhi ya wachezaji wa timu zinazocheza Ligi Kuu Tanzania wameonekana kufanya vizuri kwenye mechi za makundi, kusaka tiketi za fainali hizo.

Wachezaji hao Watanzania na wale wa kigeni wanaocheza Ligi Kuu Tanzania, wameonekana kutikisa kwenye mechi za raundi ya tano, kuwazidi hata baadhi ya wachezaji wanaocheza ligi za nchi mbalimbali Afrika na hata Ulaya.

Tanzania imeondolewa kwenye michuano hiyo, baada ya Alhamisi iliyopita kuchapwa bao 1-0 ugenini dhidi ya Equatorial Guinea na kuzima ndoto za kushiriki fainali hizo mara mbili mfululizo, huku mechi ya jana dhidi ya Libya ikiwa ni ya kukamilisha ratiba tu.

Hata hivyo, Tanzania kwenye mechi hizo za makundi, itajivunia kuwa na wachezaji mbalimbali wanaocheza ligi ambayo wamekuwa gumzo, baadhi wakizipeleka timu zao fainali za AFCON, huku vyombo mbalimbali vya habari Afrika vikiwasifia kutokana na umahiri wao.

**#1. Aishi Manula - Tanzania (Simba)**

Ni kipa namba moja wa timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars. Kwenye mechi dhidi ya Equatorial Guinea Kundi J, alikuwa nyota wa mchezo. Aliokoa michomo zaidi ya tisa ambayo wachezaji wa timu hiyo walipiga kulenga lango wakiwa ndani ya eneo la hatari.

Ingawa timu yake ilifungwa bao 1-0, Manula ambaye kwenye Ligi Kuu anaichezea klabu ya Simba, alikuwa gumzo kutokana na umahiri wake wa kuwanyima wageni nafasi ambazo zilionekana za wazi, hivyo kuwaweka roho juu, hadi dakika za mwisho ndipo walipopata bao lililowapeleka fainali za AFCON kwenye Kindi J pamoja na Tunisia, na kuinyima Tanzania nafasi.



Aishi Manula

**#2. Joash Onyango - Kenya (Simba)**

Beki huyu ambaye kwa sasa ni kipenzi cha mashabiki wa klabu ya Simba nchini, aliichezea timu yake ya Taifa ya Kenya, Harambee Stars mechi ya kufuzu dhidi ya timu ya Taifa ya Misri, Alhamisi nchini Kenya na kutoka sare ya bao 1-1.

Onyango alikula sahani moja na Mohamed Salah na hakufurukuta, na mara kwa mara alionekana kuokoa hatari nyingi, ikiwa ni kwa kuruka naye mipira ya vichwa na kumuwahi kabla ya mpira kumfikia miguuni, ambapo anakuwa hatari zaidi.

Ingawa Kenya haikufanikiwa kutinga AFCON kwenye Kundi G, Misri na Comoro zikichukua nafasi, lakini mchezaji huyo anayecheza Ligi Kuu Tanzania alitamba vilivyo.

**#3. Haruna Niyonzima - Rwanda (Yanga)**

Alilikamata dimba la kati kwenye mechi ambayo timu yake ya Taifa ya Rwanda ikicheza dhidi ya Msumbiji kwenye mechi ya Kundi F.

Niyonzima ambaye anaichezea klabu ya Yanga nchini, aliisaidia timu yake kupata ushindi wa bao 1-0 ikiwa nyumbani, Jumatano iliyopita dhidi ya Msumbiji na kuweka hai matumaini ya nchi yake kutinga AFCON kama itaifunga Cameroon kwenye mechi ya mwisho jana.

**#4. Clatous Chama - Zambia (Simba)**

Chama akiwa na timu yake ya Taifa ya Zambia, alifunga bao moja, timu yake ikitoka sare ya mabao 3-3 dhidi ya Algeria kwenye mechi ya Kundi H, Alhamisi iliyopita.

Kiungo huyo anayeichezea Simba, pamoja na kufunga bao hilo hakuiwezesha timu yake kutinga AFCON, badala yake ilishindwa na Algeria na Zimbabwe kutinga fainali hizo, huku yeye akitia fora katikati ya uwanja na kuwa mmoja wa wachezaji wa Ligi Kuu Bara waliotamba kwenye michuano hiyo.

**#5. Saido Ntibazonkiza - Burundi (Yanga)**

Kiungo anayeichezea Yanga, Saido Ntibazonkiza, Ijumaa iliyopita alifunga bao moja na kuisaidia timu yake ya Taifa ya Burundi kutoka sare ya mabao 2-2 nyumbani dhidi ya Afrika ya Kati, mechi ya Kundi E, na kusubiri hatima ya kucheza Fainali za Mataifa ya Afrika kwenye mechi ya mwisho kesho.

Ntibazonkiza na wenzake watakuwa na kibarua kizito Jumanne, Machi 30 watakapokuwa nchini Morocco kucheza dhidi ya timu hiyo na itahitaji ushindi ili iweze kufuzu, kwani itafikisha pointi tisa, lakini ikiombea Mauritania ambayo nayo itakuwa ugenini dhidi ya Afrika ya Kati ifungwe.

**#6. Perfect Chikwende - Zimbabwe (Simba)**

Straika Perfect Chikwende anayeichezea klabu ya Simba nchini, juzi alifunga bao pekee lililoipeleka Zimbabwe kwenye Fainali za AFCON mwakani nchini Cameroon.

Chikwende aliyesajiliwa na Simba kipindi cha dirisha dogo akitokea FC Platinum ya nchini humo, alifunga bao dakika ya 15 ya mchezo na kuifanya Zimbabwe kushinda bao 1-0 ikiwa ugenini dhidi ya timu ya Botswana.

**#7. Meddie Kagere - Rwanda (Simba)**

Kinara huyu wa mabao kwa sasa na mfungaji bora mara mbili mfululizo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, Jumatano iliyopita alikuwa msaada kwa timu yake ya Taifa ya Rwanda, ikishinda bao 1-0 dhidi ya Msumbiji.

Kwenye mechi hiyo iliyochezwa nchini Rwanda, iliweka rekodi ya kuwa na wachezaji watatu wa kigeni wanaocheza Ligi Kuu Tanzania Bara. Kagere mwenyewe na Niyonzima akiichezea Rwanda na kuwika vilivyo, huku Luis Miquissone anayeichezea Simba, akiwa na kikosi cha Msumbiji.

**JE, WAJUA?**



MSHAMBULIAJI wa Klabu ya Yanga na timu ya Taifa ya Burundi, Saidi Ntibazonkiza, Victor Osimhen (Napoli/Nigeria), Percy Tau (Brighton & Hove Albion/Afrika Kusini), Louis Mafouta (Neuchâtel Xamax/Afrika ya Kati) ndio wachezaji wanaoongoza kwa ufungaji wa mabao kwenye mechi za kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) zitakazofanyika mwakani nchini Cameroon, kila mmoja akiwa na mabao manne kabla ya mechi za jana.



# UVCCM kumpa ushirikiano Rais Samia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), umeahidi kumpa ushirikiano Rais Samia Suluhu Hassan ili kutimiza majukumu yake kikatiba na kutatua kero zinazowakabili vijana ikiwamo riba kubwa kwenye mikopo ya elimu ya juu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Mwenyekiti wa UVCCM, Taifa, Kheri James, alisema ni wakati wa kushikamana vijana na kushirikiana ili Rais Samia atimize majukumu ya kikatiba ya kuongoza taifa na kushughulikia manung'uniko ya kuwapo kwa riba kubwa ya mikopo hiyo.

Alisema wanaamini kwa kushirikiana na Rais Samia atashughulikia kero zinazowakabili vijana na kulipatia ufumbuzi suala hilo.

"Tukishirikiana naye rais tutampa muda mzuri wa kushughulikia kero hizi za elimu ya juu na kuweka mazingira mazuri kwa vijana, kama hatutashirikiana naye atakuwa msuluhishi wa migogoro badala ya kupanga mipango," alisema.

Alisema kutokana na dhamira ya rais ya kujenga umoja na kufungua ukurasa mpya nchini, UVCCM wanaomba radhi kama kuna kikwazo kilifanyika huko nyuma ili isiwe sababu ya kutompa ushirikiano rais wa sasa.

"Yule Magufuli (Hayati Rais John Magufuli) aliyekuwa anawatetea na kuwalea vijana ni kwasababu alikuwa na msaidizi ambaye kwa sasa amepewa jukumu la kuongoza taifa letu," alisema.

Alisema Rais Samia ataendelea kuwa kiongozi mtetezi na kuwalea vijana na kufikisha taifa sehemu ambayo inapaswa kufika.

"Ni mama anayejali, anayelea vijana, tunaye rais imara madhubuti na yupo tayari na imara kupokea majukumu haya, jukumu letu vijana ni kumuunga mkono rais wetu," alisema.

Pia alisema vijana wanajukumu la kuwaleta Watanzania wote pamoja na hawatakuwa kikwazo kwa dhamira ya rais.

"Vijana tujitahidi kuhakikisha dhamira hii njema ya kuupata ukurasa mpya ambao rais wetu anasema inafikiwa, tuna uhakika Rais Samia atatuongoza vyema," alisema.

Aliomba radhi kwa rais kama kuna mambo yalifanyika ya kuteteresha umoja wao na watahakikisha maneno na matendo yao yanaendana na dhamira ya rais wa sasa.

"Kwenye ilani ya uchaguzi kuna mambo yamezungumzwa kuhusu vijana na yaliyosemwa na Hayati Magufuli kwenye kampeni zake yatatekelezwa chini ya Rais Samia," alisema.



Mhasibu wa Mradi Jumuishi wa shirika linalohudumia watoto wenye ulemavu la Tanzania Sheshire Foundation mkoani Dodoma, Anna Pusse, akipokea cheti ya utumishi bora kutoka kwa Mratibu wa Elimu Malaamu Wizara ya Elimu, Magrert Mathonya, kwenye mkutano kuhitimisha mradi huo uliofanyika juzi Dodoma. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Watakiwa kutumia fursa ya mikopo kujikwamua

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

VIJANA wametakiwa kutumia fursa ya mikopo inayotolewa na serikali kupitia makundi mbalimbali ili kujikwamua kiuchumi.

Mkurugenzi wa Taasisi isiyo ya serikali Endless Success Foundation, Amina Feruz, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza kuhusu umuhimu wa mikopo inayotolewa na halmashauri nchini.

Alisema serikali imetenga asilimia 10 ya mikopo kwa makundi ya vijana wanawake na watu wenye ulemavu ili kuwasaidia kukuza mitaji yao na kuendeleza shughuli za ujasiriamali badala ya kutegemea ajira pekee kuendesha familia zao.

Aliwataka vijana ambao bado hawajaunda vikundi waungane kuchangamkia fursa hiyo ambayo itawasaidia kuwapa mwongozo wa kubadili fikra potofu ya kusubiri kuajiriwa wakati kuna fursa nyingi za kujiajiri kupitia ujasiriamali. "Vijana tumieni fursa ya mikopo inayotolewa na serikali kupitia halmashauri kubuni miradi ya kufanya, hii itawasaidia kujikwamua kiuchumi badala ya kusubiri ajira," alisema Feruz.

Alisema taasisi ipo kwa ajili ya kuwapa mwongozo vikundi vya vijana ya namna ya kupata mikopo hiyo ikiwamo kuwakutanisha na wataalamu kulingana na mradi wanaohitaji kufanya kwa ajili ya kuendeleza biashara wanayotarajia. "Taasisi yetu hufanya kazi ya kutoa elimu ya usimamizi wa fedha kwa vikundi vya vijana ambao wapo katika taratibu za uchukuaji mikopo ya kufanyia biashara zao za kila siku," alisema.

Alipongeza halmashauri kwa kubadili kanuni za utoaji mikopo kwa vijana ambayo itachangia vijana kubuni mawazo ya kufanya biashara ambazo zitawapa matokeo chanya. Alisema vijana wengi wana uwezo wa kufanya biashara katika maeneo wanayotoka, lakini tatizo kubwa linalowakabili ni ukosefu wa mitaji na hivi sasa serikali imewarahisishia badala kuwa na biashara wanawasilisha wazo lenye michanganuo. "Mabadiliko ya sheria hii yatawasaidia sana vijana kuendesha ujasiriamali badala ya kukaa vijiweni, hivi hakuna sababu ya vijana kulalamika kinachotakiwa ni kubuni wazo lenye tija ambalo litawasaidia kupata mkopo na kuendesha biashara walizo kusudia kufanya," alisema.

Alisema kutokana na taifa kuwa kwenye uchumi wa kati, vijana wanapaswa kutumia nafasi hiyo kuendelea kukuza uchumi kupitia biashara wanazofanya.

## Mashirika yaombwa kukatia watoto bima ya afya

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Leonard Cheshire linalofanya kazi kwa kushirikiana na Taasisi ya Tanzania Cheshire Foundation (TCF), limeomba mashirika, taasisi na watu binafsi kujitokeza kuwakatia bima ya afya watoto wenye ulemavu ili wamudu matibabu hospitalini.

Mshauri wa Elimu Jumuishi wa Shirika hilo linalofanya kazi na Taasisi ya Tanzania Cheshire Foundation, Mkoa wa Dodoma, Mtinduli Mwalongwe, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na wadau kutoka taasisi zisizo za kiserikali na viongozi wa idara za serikali kwenye mkutano wa kuhitimisha mradi wa elimu jumuishi uliofanyika Dodoma.

Mwalongwe alisema wazazi wengi wenye watoto wenye ulemavu wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa bima ya afya na kulazimika kuwafungia kwa kukosa matibabu.

"Moja ya kero waliyokuwa nayo wazazi na walezi wenye watoto wenye ulemavu ni namna ya kukabiliana na matibabu ya watoto hao, kwa kuwa wengi wao hawana fedha za kukatia bima ya afya," alisema.

Alisema watoto hao wanahitaji kupatiwa huduma ya afya hospitali, tatizo lililopo ni gharama kubwa wanayokutana nayo ambayo hata hivyo wanashindwa kuimudu, hali ambayo inayowafanya wazazi hao kurudi nyuma na kuamua kuwaficha ndani.

"Serikali kwa kushirikiana na mashirika, taasisi na watu binafsi mradi unawaomba kujitokeza kuwakatia bima ya afya ili kutibiwa na kupata matibabu ya uhakika kutokana na aina ya ugonjwa," alisema.

Akitoa maelezo ya jinsi unavyotekeleza miradi ya elimu jumuishi kupitia taasisi ya Tanzania Cheshire Foundation (TCF), kwa ajili ya kuwawezesha maendeleo ya watu wenye ulemavu, Mratibu na Meneja wa mradi huo Manance Mhambwe, alisema kwa sasa umefikia shule 20 za halmashauri za Chamwino na Dodoma.

Mhambwe alisema kuwa lengo la mradi huo ni kuhakikisha wanawabaini na kuwatambua watoto wenye ulemavu ili kufikia malengo ya kuwafikia watoto wenye ulemavu na kuboresha mazingira ya kujifunzia ili kuhitimu elimu ya msingi.

Mradi huo umekuwa ukifanya kazi zake kusaidia vifaa mbalimbali kwa ajili ya watoto wenye ulemavu, kama vile visaidizi na mahitaji muhimu ya shule ikiwamo miwani, baiskeli mwendo, mafuta ya watu wenye ualbino, sare, kalamu na madaftari.





Baadhi ya wakulima katika Bonde la Usangu, wilayani Mbarali, katika Mkoa wa Mbeya, wakiendelea na shughuli za upandaji miche ya mpunga juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# 'Muenzini JPM kuwafunza watoto uzalendo'

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JAMII imeshauriwa kumuenzi Hayati Dk. John Magufuli kwa kuwapatia watoto malezi bora yatakayowaandaa kuwa wazalendo na mashujaa ili kuliletea maendeleo Taifa la Tanzania.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa mapadre Jimbo la Katoliki Mkoa wa Mbeya, Padri Gaspar Mwangoka, wakati akizungumza na Nipashe mambo yanayopaswa kufanya wananchi ili kumuenzi Hayati Dk. Magufuli.

Alisema eneo la malezi ndio sehemu pekee itakayoweza kuwaandaa vijana wazalendo wa kuja kulitumikia taifa kwa uadilifu kama alivyokuwa Hayati Dk. Magufuli na wazazi na walezi wanapaswa kulisimamia suala hilo kikamilifu.

"Yatupasa kuwaandaa vijana wetu kuwa wazalendo na wapenda nchi zao, hili tutalifanikisha endapo tunazingatia malezi bora yanayoakisi utamaduni wetu, tutazalisha kina Magufuli wengi Afrika na Tanzania kwa sababu alikuwa ni Rais mzalendo kwa nchi yake," alisema Padri Mwangoka.

Kwa upande wake, Shehe Ibrahim Bombo, alisema watoto wanahitaji malezi na mwongozo mzuri kwa kuhakikisha wazazi wanalisimamia hilo badala ya kuwaachia wasaidizi wao wa kazi nyumbani.

Alisema watoto wa siku hizi wanakosa malezi bora kutokana na wazazi kuwa bize na shughuli za uzalishaji kama vile ujasiriamali na kusahau jukumu la kulea familia.

Askofu wa Kanisa la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKT) Dayosisi ya Konde, Edward Mwaikali, alisema jukumu la malezi sio tu la wazazi bali hata viongozi wa dini kupitia mafundisho yao wanapaswa kuwafundisha watoto au vijana namna bora wa kuwa wenye utii wazalendo na wenye kuzingatia maadili.

Alisema kwa sasa taasisi za dini zinaandaa mafundisho kwa wazazi na vijana ili kuwaelekeza mambo yapasayo kwenye jamii na ya kumpendeza Mungu.

# Serikali yaahidi kusimamia miradi ya maendeleo Mbeya

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

SERIKALI mkoani Mbeya imeahidi kusimamia na kuilinda miradi mbalimbali ya maendeleo inayoendelea kujengwa ili thamani ya fedha iliyotumika iendane na miradi, lengo likiwa ni kukabiliana na vitendo vya rushwa.

Kauli hiyo ilitolewa hivi karibuni na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila wakati akikagua utekelezaji wa miradi katika wilaya za Kyela na Rungwe.

Alisema pia wananchi wanatakiwa kuwa walinzi na kuipa thamani miradi yote inayotekelezwa na serikali ikiwa ni pamoja na kuitunza miundombinu kama vile ya miradi ya maji.

Aliwataka wananchi kuchangia miradi inayoletwa na serikali ili itekelezwe kwa haraka kama vile kutoa baadhi ya maeneo ya kijiji.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maji, Meneja wa Mamlaka ya Maji, Mhandisi, Tanu Deule, alisema hadi mradi wa maji wa Matema utaohudumia vitongoji vya Ibungu na Lyulilo, umetumia Sh. milioni 344.

Mradi mwingine ni Mababu ambao hadi sasa kiasi cha Sh. milioni 90 kimetumika bado ujenzi unaendelea.

Mhandisi Deule alisema kukamilika kwa miradi yote hiyo kunahitaji Sh. milioni 29 kitatumika.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Claudia Kitta, alisema baadhi ya wananchi wameanza kupata huduma ya majisafi na salama kupitia mradi Matema na kwa miaka 10 hawakuwahi kupata huduma hiyo.

Katika hatua nyingine Kitta alisema wilaya hiyo imefanikiwa kujenga mabweni matatu na bwalo kwenye Shule ya Sekondari Kafundo, Kata ya Ipinda.

Aliwahimiza wazazi kuchangia chakula shuleni ili wanafunzi wasome kwa furaha na kuwa na ufikiri mzuri katika masomo yao wawapo darasani.

# Mbarali yamaliza mgogoro wa wafugaji

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, imemaliza mgogoro baina ya wafugaji wa vijiji vya Magigiwe, Iwalanji, Mapogoro, Igunda Magwali, Luhanga na Iyala na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha wa kukamata mifugo na kulipisha faini Sh. 100,000 kwa kila mfugo unaoinga katika maeneo wanayodai kuwa sio ya hifadhi.

Mgogoro huo ulimalizwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu hatua zilizochukuliwa hadi sasa kukabiliana na uvamizi kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Wafugaji walimweleza Mfune kuwa wamekuwa wakitozwa faini kwenye maeneo ambayo sio ya hifadhi, kutokana na maelezo hayo aliagiza kusitisha mgogoro huo na kuzitaka pande zote mbili kutumia busara ili kuepusha malalamiko na kusisitiza kila mmoja kutimiza majukumu yake bila kuvunja sheria.

"Naomba mgogoro huu usitishwa, wafugaji wasitozwe tena faini wala mifugo yao kukamatwa, uongozi wa hifadhi ya Ruaha mwendelee kutoa elimu kwa wakulima na wafugaji bila kukoma ili kila mmoja afahamu mipaka yake, wakati serikali ikiendelea na mchakato wa upatikanaji wa suluhu ya kudumu ambao upo katika hatua za mwisho za umaliziwaji wake," alisema Mfune.

Mfune alisema uamuzi wa kusitisha mgogoro huo utasaidia viongozi wa kata, vijiji na hifadhi kukaa meza moja kuonyesha maeneo ya msingi ambayo yalikwishalipwa fidia na ambayo bado hayajalipwa ili wafugaji waweze kujua wanaishia wapi wanapokwenda kulisha mifugo yao wakati wakisubiri maelekezo ya mwisho ya mpaka wa kudumu kutoka serikali kuu.

Alisema halmashauri tayari ilainisha maeneo yote ya mpaka na maeneo ambayo watu walishalipwa kwamba hairuhusiwi kuingiza mifugo na kwamba kwa wale watakaotaka kukiuka utaratibu huo tutawachukulia hatua kwa mujibu wa sheria.

Baadhi ya wafugaji walisema kwa muda mrefu mifugo yao ilikuwa ikikamatwa kwa sababu ya kutofahamu mipaka inapoishia na kutokana na maelezo ya mkuu wa wilaya kila mmoja ataheshimu na kufuata sheria zilizowekwa.



# Mufti afunda maimamu kuhusu utulivu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAIMAMU wa misikiti na masheha wametakiwa kuendeleza falsafa ya viongozi wakuu wa Zanzibar ya kuimarisha amani na utulivu baada ya maridhiano ya kisiasa yaliyofikiwa na viongozi hao.

Mufti wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kaabi, aliyasema hayo kwenye mkutano wa maimamu na masheha wa Wilaya ya Kusini Unguja ulioandaliwa na ofisi yake kwa kushirikiana na Taasisi ya Marafiki wa Zanzibar katika Ofisi ya Halmashauri Kitogani Kusini Unguja.

Alisema hali ya amani na mshikamano wa wananchi wa Zanzibar ni nzuri, lakini maimamu na masheha wana jukumu la kuiendeleza na kuisimamia kwa sababu wana kundi kubwa la watu wanaowangoza na wao ndio chanzo cha amani.

Mufti huyo alisema suala la kutunza amani na mshikamano lisiishie kwa viongozi wa juu bali kila mtu anapaswa kutumia nafasi aliyonayo katika kusimamia suala hilo. Naye Katibu Mkuu wa Taasisi ya Marafiki wa Zanzibar, Dk. Aboubakar Kabwogi, alisema Zanzibar imekuwa nchi ya kuigwa na mataifa mengine kwa kufikia muafaka wa kisiasa ambao umeleta amani na kuharakisha maendeleo.

Akitoa mchango katika mkutano huo, Imamu Mkuu wa Msikiti wa Mzuri Makunduchi, Sheikh Habibu Mohamed Mussa, aliwashauri viongozi wa juu kuwa na msimamo wa dhati wa maridhiano yaliyofikiwa kwani ndio kigezo chao. Aidha, washiriki wa mkutano huo walishauri kuendelezwa utaratibu wa viongozi wakuu kuswali sala za Ijumaa katika misikiti tofauti kwa vile inahamasisha kuendeleza amani na umoja kwa wananchi wote.

# 'Wanawake walindeni watoto dhidi magonjwa ya kujamiiana'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAWAKE wametakiwa kuwalinda watoto wao dhidi ya magonjwa yanayotokana na kujamiiana katika umri mdogo ili kuepukana na athari hizo.

Hayo yalielezwa na daktari bingwa wa afya ya mama na mtoto kutoka Hospitali Kuu ya Mnazimmoja Zanzibar, Ummukulthum Omar Hamad, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema kufanya hivyo pia kutawawezesha kujitambua na kuepuka vishawishi vitakavyohatarisha afya zao.

Alisema watoto wamekuwa wakijiingiza katika vitendo vya kujamiiana bila kutambua athari wanazoweza kuzipata ikiwamo mimba za mapema na athari wakati wa kujifungua pamoja na kupata magonjwa ya gono ukiwamo Ukimwi.

Dk. Ummy alieleza kuwa kulingana na wakati uliopo sasa kuna haja ya wazazi kubadilika katika malezi kwa kuwa karibu na watoto na kuwapa faida za kulinda bikira yao kwa kutokubali kuchezewa kimwili hadi wakati husika utakapofika.

Aidha, alishauri umuhimu wa wanafunzi kujengwa mapema kisaikolojia tokea wakiwa shuleni kwa sababu wanafunzi wengi wamekuwa wakiharibu malengo yao ya kielimu kwa kuingia katika vitendo hivyo kabla ya wakati.

"Wapo wanafunzi wanapata ujauzito licha ya sheria kuruhusu kuendelea na masomo, lakini wengi wao huwa hawaendelei kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo aibu," alisema.

Hata hivyo, alisema ni vyema wanafunzi wakapatiwa elimu ya afya ya uzazi toka wakiwa shuleni ili kujua athari za mimba za utotoni na athari ambazo wanaweza kuzipata wakati wa kujifungua.



Waumini wa Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Joseph Mjini Zanzibar wakiadhimisha sikukuu ya Matawi, mwanzo wa fumbo la Pasaka, jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Katibu Mkuu Kiongozi amfagilia Rais Samia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhandisi Zena Ahmed Said, amesema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, amejengwa katika misingi mizuri ya kuongoza Tanzania kutokana na kupata uzoefu wa kufanya kazi na marais mbalimbali wastaafu.

Aliyasema hayo baada ya kutia saini kitabu cha maombolezo cha aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli hapo katika ukumbi wa Shekhe Idrisa Abdulwakil Kikwajuni Zanzibar.

Alisema hiyo ni fursa kubwa ya kipekee ambayo inaweza kutumika kupima uwezo kwa wanawake katika sifa za uongozi wa ngazi za juu.

Alisema Rais Samia amebahatika kupata uzoefu wa uongozi katika ngazi tofauti ukianzia na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo ameshika nafasi mbalimbali za juu za uongozi.

Alisema katika nafasi hizo kwa kiasi kikubwa amefanya kazi na viongozi wa ngazi za juu wa serikali na kuwa na mbinu za kuongoza.

Alisema alipokuwa Zanzibar alipata nafasi ya kushika nyadhifa mbalimbali za juu za uongozi ikiwamo Waziri wa Vijana, Wanawake na Watoto kabla ya kushika nafasi ya Waziri wa Utalii, Biashara, na viwanda wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa miaka kumi.

"Sina wasiwasi na uongozi wake wa ngazi za juu...amepata kuongoza Zanzibar na kushika nafasi mbalimbali hadi Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo kwa kipindi cha miaka mitano alipata kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano chini ya Hayati Rais Magufuli," alisema Zena.

Aidha, alisema akiwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amepata kushika nafasi mbalimbali akiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia mambo ya Muungano na kwa kiasi kikubwa ni kiongozi anayeifahamu vizuri Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na tunu zote za kitaifa ziliopo.

Alisema matarajio yake makubwa ni kwamba Muungano wa Tanganyika na Zanzibar upo salama na utaendelea kudumishwa kwa nguvu zote katika kipindi cha uongozi wa Rais Samia.

"Nimejenga matumaini makubwa na uongozi wake....ni Rais anayeifahamu vizuri Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwamo Zanzibar pamoja na kufanya kazi na marais wastaafu wa Zanzibar na Muungano, kwa hivyo amechota busara na fikra za uongozi...Muungano wetu upo katika mikono salama," alisema.

Baadhi ya makatibu wakuu waliopata kufanya kazi na Rais Samia wamewatoa wasiwasi wananchi kwamba uwezo wa kuongoza anao mkubwa, huku akiwa kiongozi mwenye busara, hekima na kufanya maamuzi yaliyohakikiwa vizuri.

Omar Dadi Shajak, aliyekuwa Katibu Mkuu Wizara ya Vijana, Wanawake na Watoto huku waziri wake akiwa Samia, mwaka 2000, alisema ni kiongozi aliyetulia mwenye kumsikiliza kila mtu akiwamo watumishi wake, huku akifanya maamuzi yaliyohakikiwa vizuri bila ya jazba.

Alisema katika kipindi hicho walifanikiwa kujenga misingi mizuri na kutayarisha sheria nzuri kwa ajili ya wanawake na watoto ambazo zilipata sifa na kutambuliwa kimataifa.

"Tumepata rais mwenye sifa zinazojitosheleza, ambaye ana uwezo mkubwa wa kuongoza kwa kufuata misingi ya hekima, busara na kujengwa na uadilifu mkubwa," alisema Shajark ambaye kwa sasa ni Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wanawake na Watoto.

HABARI KITAIFA

# CAG aanika ripoti zenye hati chafu, safi

Na Elizabeth Zaya

MKAGUZI na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, amesema kati ya hati za ukaguzi 900 zilizotolewa na ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, 10 ni mbaya, 81 zina mashaka na 800 zinaridhisha.

Pia alisema hati tisa kati ya hizo, alishindwa kuzitolea maoni kama sheria inavyompa mamlaka ya kufanya hivyo baada ya ukaguzi.

Alisema kati ya hati 900 zilizokaguliwa kwa kipindi hicho cha mwaka wa fedha 2019/2020, za serikali kuu ni 243, serikali za mitaa 185, mashirika ya umma 165, miradi ya maendeleo 290, na vyama vya siasa 17.

Alisema hayo jana wakati akikabidhi taarifa ya ukaguzi wa Mashirika na Taasisi za Umma kwa Rais Samia Suluhu Hassan, jana Ikulu Chamwino, jijini Dodoma.

**TAMISEMI**

Alisema amekagua mamlaka za serikali za mitaa 185 na kati ya hizo zenye hati zinazoridhisha ni 124, zenye mashaka 53 na mbaya ni nane.

**MASHIRIKA YA UMMA**

Mashirika ya umma yaliyokaguliwa ni 165, kati ya hayo 162 ndiyo yenye hati zinazoridhisha na tatu ni zenye mashaka.

**SERIKALI KUU**

Kichere alisema hati 243 zimetolewa katika Serikali Kuu na kati yake 235 zinaridhisha, zenye mashaka sita na mbaya ni mbili.

**VYAMA VYA SIASA**

Hati zilizokaguliwa ni 17, zinazoridhisha ni nne, zenye mashaka ni nne huku kukiwa na vyama visivyokuwa na hati mbaya na baadhi havikupeleka hesabu zao kukaguliwa.

"Kwenye vyama vya siasa tisa nilishindwa kutoa maoni kutokana na hesabu zao kutozingatia utaratibu wa kutengeneza hesabu na wengine hawakuleta kabisa hesabu ili nizikague," alisema Kichere.

**MIRADI YA MAENDELEO**

Alisema miradi iliyokaguliwa ni 290, kati ya hiyo yenye hati za kuridhisha ni 275, yenye hati za mashaka ni 15, na hakukuwa mbaya.

Kichere aliiomba serikali kuhakikisha inafanyia kazi mapendekezo mbalimbali yanayotolewa na ofisi hiyo.

**RIPOTI ZILIZOWASILISHWA**

Alitaja miongoni mwa ripoti zilizowasilishwa kuwa ni ya ukaguzi wa serikali kuu, Mamlaka ya Serikali ya Mitaa, Mashirika ya Umma, miradi ya maendeleo, ripoti ya ukaguzi wa ufanisi, ripoti ya ukaguzi wa mifumo wa TEHAMA.

Nyingine ni ripoti ya ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti ya ukaguzi wa ufanisi kwa miaka iliyopita pamoja na ripoti 14 ya ukaguzi wa ufanisi zinazohusu sekta mbalimbali.

Katika ripoti hizo, alisema ipo ya ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa usafi wa masoko ya vyakula, ukaguzi wa ufanisi juu ya usimamizi wa udhibiti wa mafuriko, ukaguzi wa ufanisi kuhusu uandikishaji na utoaji wa vitambulisho vya taifa.

Ripoti nyingine ni ya ukaguzi wa ufanisi kuhusu matengenezo ya magari na mitambo ya serikali, ukaguzi wa ufanisi kuhusu usimamizi na ununuzi wa pamoja wa magari ya serikali na usambazaji wa mafuta, ukaguzi wa ufanisi ya usimamizi wa mifumo wa kudhibiti ubora wa vyakula vinavyosindikwa nchini.

Mwingine ni ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa ujenzi wa majengo ya vituo vya huduma za afya nchini, ukaguzi wa ufanisi wa mali zilizotelekezwa.

Pia ukaguzi wa ufanisi wa utekelezaji wa udhibiti wa uhamishaji wa bei ya mauziano ya bidhaa au huduma baina ya kampuni zenye uhusiano na ukaguzi wa ufanisi wa ufuatilijia na usimamizi wa miradi ya ujenzi kwenye sekta ya elimu inayotekelezwa kwa njia ya 'force' akaunti.

Ukaguzi mwingine alisema ni ya udhibiti wa uchafuzi unaotokana na taka za plastiki kwenye bahari na maziwa, ukaguzi wa ufanisi kuhusu utekelezaji wa mradi wa awamu ya pili ya ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo kwa haraka Dar es Salaam (DART), usimamizi wa misamaha ya kodi kwenye miradi ya uwekezaji na utekelezaji wa miradi ya uzalishaji sukari Mbigiri, mkoani Morogoro.

**MIRADI YA KIMKAKATI**

Akizungumzia miradi sita ya kimkakati, Kichere alisema wametumia mbinu mpya ya ukaguzi katika miradi hiyo kazi ambayo walifanya kwa kadri mradi unavyoendelea kutekelezwa ili kusaidia kutoa ushauri kwa serikali katika kuchukua hatua mapema.

Alitaja miradi hiyo kuwa ni pamoja na mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora, mradi wa bwawa la kufua umeme la Mwalimu Julius Nyerere.

Mingine ni mradi wa barabara ya haraka ya Gerezani hadi Mbagala, upanuzi wa barabara ya Morogoro, Kimara hadi Kibaha, mradi wa usambazaji maji katika wilaya ya Same, Mwanga na Korogwe na mradi wa uzalishaji sukari Mbigiri, mkoani Morogoro.

## Wajitokeza kwa wingi uchaguzi mdogo Pemba

Na Mwandsihi Wetu, PEMBA

WANANCHI wa Jimbo la Pandani Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba, jana, walijitokeza kupiga kura katika vituo 18 vilivyomo katika uchaguzi mdogo wa kujaza nafasi ya aliyekuwa mwakilishi mteule wa wa Chama cha ACT- Wazalendo, Abuubakar Khamis Bakar, aliyafariki dunia mwaka jana.

Katika vituo hivyo vya kupigia kura idadi ya wananchi walio-jitokeza kwa wingi tofauti na uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka jana.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, aliwataka wananchi wa Jimbo hilo kutumia haki yao ya kikatiba ili kumchagua mwakilishi wao atakayewatatulia matatizo yao.

Aidha, Salama aliwataka wananchi hao baada ya kupiga kura kurudi majumbani mwao na kuendelea na shughuli zao za kujitafutia riziki badala ya kukaa katika vikundi.

Aliwaambia wananchi kuwa Serikali ya Mkoa imejipanga vizuri kuimarisha ulinzi na usalama unakuwapo.

"Ninachowaomba wananchi msiwe na hofu, msistushwe na wala msiogope, hakikisheni mnafuata taratibu na sheria zilizowekwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC)," alieleza Salama.

Mapema Salama aliwatoa hofu wananchi kuwa matokeo ambayo yatatangazwa na ZEC atakuwa ya haki na hakuna atakayedhulumiwa haki yake.

"Kwa upande wa matokeo tumejipanga vizuri ili kuona haki inatendeka kuanzia wakati wa kuhesabu kura hadi matokeo yenyewe," alisema Salama.



Mwendesha pikipiki akipita kwenye dimbwi la maji kutokana na mvua iliyonyesha juzi, katika eneo la Chanika na kusababisha ubovu wa barabara inayoelekea Msanga Zalala, huku akiwa amembeba abiria. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## HABARI KIMATAIFA

# Uganda yagawa vyandarua mil. 27

**Kampala,** UGANDA

WIZARA ya Afya Uganda, imesema imekamilisha usambazaji wa vyandarua milioni 27.5 vyenye dawa nchi kote.

Msemaji wa wizara hiyo, Emmanuel Ainebyoona, aliliambia Shirika la Habari la Xinhua, mwishoni mwa wiki na kwamba vyandarua hivyo vimeshasambazwa kwa kipindi cha miezi nane.

"Hii ilikuwa ni kampeni ya usambazaji vyandarua iliyozinduliwa Agosti, mwaka jana," alisema Ainebyoona.

Alisema kampeni hiyo ilifanyika Kaskazini, Mashariki, Kati na Magharibi mwa nchi kwenye mikoa tofauti.

"Hii inalenga kuwalinda Waganda na mbu na kukabiliana na malaria. Kama mnavyojua malaria inabaki kuwa sababu kuu ya vifo nchini," alisema Ainebyoona.

Alisema vyandarua hivyo ambavyo vilitolewa bure, wizara inatarajia wananchi waliopatiwa watatumia vyandarua hivyo ili kujikinga na malaria.

"Wizara ya Afya, imetoa kipaumbele katika ugawaji wa vyandarua ikiwa ni mbinu ya kukabiliana na malaria na imethibitishwa ni kati ya hatua gharama nafuu ya kukabiliana na ugonjwa huu," wizara ilisema hayo kwenye taarifa yaje mwishoni mwa wiki.

Kampeni hiyo imesaidia nchi kupunguza kiwango cha malaria kutoka asilimia 17 mwaka 2014 na 2015, hadi kufikia asilimia tisa mwaka 2019.

Pia hatua kadhaa zimeendelea kuchukuliwa ikiwamo upuliziwaji wa dawa kwenye makazi ya watu nchini.

**XINHUA**



Waokoaji wakitafuta watu chini ya kifusi cha jengo lililoporomoka mjini Cairo, nchini Misri, tukio lililotokea juzi na kuua watu watano huku 24 wakijeruhiwa, mjini humo. **Picha: Xinhua**

# Juhudi zaendelea kuinasua meli iliyonasa mfereji wa Suez

**Cairo**, MISRI

MELI kubwa ya mizigo ambayo bado imekwama katika mrefeji wa Suez kwa siku ya sita, juhudi nyingine zimeanza kuiondoa na kufungua njia iliyo muhimu Mashariki na Magharibi, hususani kwa usafirishaji wa bidhaa duniani.

Meli hiyo ya Ever Given yenye bendera ya Panama ambayo ilibeba mizigo ya Asia na Ulaya, ilikwama Jumanne katika mfereji huo unaopita kati ya Afrika na Peninsula ya Sinai.

Ofisa mmoja wa usimamizi wa Suez ambaye hakutaka kutambulishwa alisema mamlaka zinatarajiwa kufanya majaribio mawili kuiondoa meli hiyo.

Hata hivyo mkuu wa mfereji wa Suez, Luteni Jenerali Osama Rabei, alisema atafanya mkutano na waandishi wa habari katika mji wa Suez kutoa maelezo zaidi ya operesheni hizo.

Taarifa zilisema meli hiyo kubwa ya mizigo imesababisha kukwama kwa biashara na bidhaa zenye thamani ya dola billioni 9.6 kwa siku, kulingana na takwimu za safari za meli.

Takwimu hizo zilionyesha hasara ya dola milioni 400 kwa saa moja katika biashara inayotokana na njia hiyo, baina ya Mashariki na Magharibi.

Kampuni ya Lloyd's, inayofuatilia bidhaa zinazobebwa na meli ilisema bidhaa inayopita katika mfereji wa Suez kuelekea nchi za Magharibi, ina thamani ya dola bilioni 5.1 kwa siku, wakati zile zinazo kwenda nchi za Mashariki zina thamani ya dola bilioni nne na nusu kwa siku.

Licha ya juhudi zinazoendelea kuikwamua meli hiyo, wataalamu walisema kazi hiyo inaweza kuchukua wiki kadhaa.

Meli hiyo yenye urefu wa mita 400 sawa na viwanja vinne vya mpira wa miguu inakadiriwa meli kukwamisha meli 300 kuendelea na safari kutokana na meli hiyo.

Maofisa wa mfereji walisema kwamba wana matumaini meli hiyo ingeweza kusafiri tena ifikapo jana jioni.

**VOA**

# 114 wauawa maandamano Myanmar

**Yangon,** MYANMAR

WATU 114 wameuawa na Jeshi la Polisi Myanmar, wakati wakiandamana kupinga mapinduzi ya kijeshi yaliyofanywa dhidi ya serikali iliyochaguliwa kidemokrasia ya Aung San Suu Kyi.

Waandamanaji nchini Myanmar walirudi tena kwenye maandamano mitaani, wakishinikiza madai yao ya kutaka demokrasia irudishwe.

Ikiwa ni siku moja baada ya vikosi vya usalama kusababisha umwagaji mkubwa wa damu kwa kuwaua zaidi ya watu 100.

Umwagikaji huo wa damu ndio mkubwa zaidi kutokea tangu mapinduzi ya jeshi nchini humo, mwezi uliopita.

Maandamano siku ya jana, yameshuhudiwa Yangon na Mandalay miji miwili mikubwa nchini humo na maeneo mengine.

Baadhi ya waandamanaji walipambana tena na vikosi vya polisi.

Mapinduzi ya Februari Mosi, mwaka huu, yaliyomwondoa madarakani Aung San Suu Kyi na serikali yake iliyochaguliwa na wananchi.

Miongoni mwa waliouawa ni pamoja na watoto waliokuwa chini ya umri wa miaka 16 kwa mujibu kituo cha habari cha mtandaoni cha Myanmar.

Takwimu sawa na hiyo ya waliouawa ilitolewa pia na vyombo vingine vya habari vya Myanmar, ikiwa ni idadi kubwa ya watu waliouawa ikilinganishwa na mauaji yaliyofanyika Machi 14, mwaka huu.

Kwa ujumla waliouawa nchini humo, tangu mapinduzi ya kijeshi ni watu 420 kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali.

Mapinduzi ya Myanmar yamebadilisha kabisa hatua zilizopigwa miaka kadhaa, kuelekea demokrasia baada ya miongo mitano ya nchi hiyo kuwa chini ya utawala wa kijeshi na kuifanya tena nchi hiyo kumulikwa na Jumuiya ya kimataifa.

Umwagikaji huo wa damu umelaaniwa na jumuiya ya kimataifa kupitia ofisi za kidiplomasia ndani ya Myanmar na nje ya nchi hiyo.

**DW**



# Messi, Ronaldo sasa watakiwa Marekani

**MEXICO CITY,** Mexico

RAIS wa Ligi Kuu ya nchini Mexico, Mikel Arriola, ameeleza matamanio yake ya kuwapeleka Lionel Messi na Cristiano Ronaldo katika Ligi Kuu ya nchini Marekani, MLS.

Marekani na Mexico wanatarajiwa kuwa na ligi moja ya soka, na Mataifa hayo mawili ya Amerika Kaskazini yamekuwa yakijadili juu ya kuungana, na Arriola ana matumaini kuwa inaweza kufanyika baada ya Kombe la Dunia la 2026 litakalounganisha Marekani, Mexico na Canada.

Tayari Marekani na Canada wanacheza ligi moja ya mpira wa kikapu inayozikutanisha timu za nchi hizo mbili na sasa wanataka kugeukia kwenye soka.

Arriola pia anaamini ligi hizo mbili zinaendelea kukua, na wanaweza kusajili wachezaji hao wawili kwenye mpira wa miguu kwa zaidi muongo uliopita.

Akizungumza na ESPN, Arriola alisema: "Tungekuwa moja ya ligi bora ulimwenguni (ikiwa tutaungana na MLS).

"Hatua inayofuata itakuwa na Messi au Cristiano Ronaldo hapa (Mexico) au Marekani, labda katika hatua ya mwisho kabisa ya soka lao.

"Naamini Messi na Ronaldo wanaweza kuja kucheza hapa na kwa kiasi kikubwa wanaweza kuipeleka mbele ligi hiyo," aliongeza.





# Kipa wa Chelsea atoa tofauti Tuchel, Lampard

**LONDON,** England

GOLIKIPA wa Chelsea, Willy Caballero, ameelezea tofauti zilizopo kati ya kocha wa zamani wa Chelsea, Frank Lampard na bosi wa sasa Thomas Tuchel akiwa ametumia muda wake kuwa na makocha hao.

Tuchel alichukua mikoba kwa Lampard Januari baada ya kiungo huyo wa zamani wa Chelsea kufukuzwa kutokana na mwenendo mbaya wa timu.

Caballero amesema Tuchel ana tofauti sana kuliko mtangulizi wake hasa kwenye soka la kisasa.

"Kimsingi kuzungumzia kuhusu makocha, kuwa mmoja amefanya vizuri na mwingine amefanya vibaya si jambo zuri," alisema Caballero akiiambia 90min.com.

"Kwa sababu wote wameitumika Chelsea na wote ni walimu wazuri wanaushawishi kwenye soka.

"Bila shaka tulipokuwa na Lampard tulikuwa na mawazo ya moja kwa moja hasa kwa soka la Kiingereza, kushambulia haraka, mashambulizi ya pembeni na katikati.

"Sasa na Tuchel, anatumia mbinu ya kucheza kwa pamoja, kumiliki mpira, tunatengeneza nafasi nyingi mara nyingi amekuwa akituambia jinsi ya kuendeleza na kuwasoma wapinzani sehemu gani ni muhimu, kwa maana ya uimara wao na udhaifu wao.

Tuchel tangu achukue mikoba ya kuinoa Chelsea Januari mwaka huu, ameshinda michezo 10 na kutoa sare mechi nne katika michezo 14 ya Premier League na kwa sasa Chelsea wamekaa katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo.



# Pjanic: Nataka kupigania namba hapa Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

MIRALEM Pjanic amepanga kubaki na kupigania namba yake pale Barcelona licha ya kuanza vibaya pale kwenye dimba la Camp Nou.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Bosnia-Herzegovina, Pjanic alijiunga na Barca mwaka jana huku kiungo mwenzake, Arthur akienda upande mwingine kule Juventus.

Lakini Pjanic hajawa na wakati mzuri chini ya kocha, Ronald Koeman pale Barcelona na hajawa na namba ya kudumu katika kikosi hicho.

Kiwango bora cha Pedri kimemfanya kuwa kwenye nafasi ya kuanza mara kwa mara, huku nyota huyo mwenye umri wa miaka 30, na Pjanic kushindwa kupata nafasi ya kutosha.

Hata hivyo, Pjanic ameiambia Mundo Deportivo hana mpango wa kwenda popote, kwani anawania kupambania namba yake hapo.

"Sikusajiliwa Barca ili niondoke mwaka unaokuja," alisema Pjanic wakati akizungumzia kuhusu uvumi wake wa kutaka kuondoka.

"Nilisaini kutengeneza historia kwenye klabu hii na naamini nitakuwa hivyo ii niweze kufanya vizuri."

## HABARI MICHEZO

# Vidal anogewa Inter Milan




**MILAN,** Italia

ARTURO Vidal amepokea ofa ya kuondoka Inter Milan, lakini anapanga kubaki pale San Siro na kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, kwa mujibu wa wakala wa kiungo huyo, Fernando Felicevich.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Chile alijiunga na Inter akitokea Barcelona mwanzoni mwa msimu huu kuungana na Antonio Conte, awali akiwa amefanya naye kazi kule kwa miamba wa Serie A, Juventus ambapo kwa pamoja walishinda mataji mara tatu ya Ligi Kuu.

Amecheza mechi 30 kwenye mashindano yote katika kikosi cha Conte msimu huu, lakini alikumbwa na majeraha ya goti mapema mwezi huu na kulazmika kufanyiwa upasuaji.

Vidal bado ana miaka miwili imebaki kwenye mkataba wake wa sasa, lakini uvumi haujakoma kwamba anawaniwa na klabu kama Marseille, Flamengo na Galatasaray.

Lakini wakati klabu hizo zikionyesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, wakala wake, Felicevich amesisitiza mteja wake hana mpango wa kuondoka kwa miamba hao wa Italia mwishoni mwa msimu huu.

"Ni kawaida kwa mchezaji wa daraja la juu kama Arturo kupata ofa ya kuwaniwa, lakini hakuna kilichobadilika," alisema Felicevich akiliambia gazeti la La Gazzetta dello Sport.

"Majaliwa yake yapo pale Inter na anafikiria kushinda Scudetto Mei mwaka huu na kujaribu kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao."

Vidal amecheza mechi 23 kwenye Serie A msimu huu, 14 kati yake akianza na kuisaidia Inter kuongoza msimamo kwa tofauti ya pointi sita dhidi ya AC Milan.

## Ronaldo bado yupo sana Juve

**TURIN,** Italia




CRISTIANO Ronaldo ataendelea kubaki kuichezea Juventus hadi mwishoni mwa mkataba wake, hiyo ni kwa mujibu wa Makamu Rais wa klabu hiyo, Pevel Nedved.

Nedved ameyaweka hayo wazi baada ya kuwa na tetesi kuwa raia huyo wa Ureno ataondoka mwishoni mwa msimu huu kujiunga na Real Madrid.

Ronaldo amekuwa akikosolewa na baadhi ya wachambuzi na mashabiki kwa kutokuwa na msaada kwa timu yake katika michuano ya Ulaya na ile ya Serie A.

"Ana mkataba hadi Juni 30, 2022 na ataendelea kuwa nasi katika kutimiza majukumu yake," alisema Nedved akinukuliwa na Sky Sport Italia.

"Kwangu mimi, Cristiano hawezi kuguswa na yeyote katika usajili."

Kiongozi huyo ambaye pia ni kiungo wa zamani wa Juventus na timu ya Taifa ya Czech, ameongeza kuwa kocha wa timu hiyo, Andrea Pirlo, ataendelea kubaki kuongoza kikosi hicho.

"Pirlo ataendelea kuwa kocha wa Juventus, huo ni uhakika asilimia 100," alisema Nedved.

## Lukaku awindwa tena Chelsea

**LONDON,** England

KLABU ya Chelsea imeongeza jina la mshambuliji wao wa zamani, Romelu Lukaku kama mmoja wa washambuliaji inaowania kutua katika viunga vya Stamford Bridge.

Kwa mujibu wa Sky Sport, Chelsea sasa wanaona Lukaku anaweza kuwa nyota muhimu kwenye kikosi hicho na hivyo wanawania saini yake kipindi cha majira ya joto.

Chelsea wanamtazama Lukaku kama chaguo namba moja, endapo watashindwa kuinasa saini ya mshambuliaji kinda wa Borussia Dortmund, Erling Haaland ambaye anamezewa mate na klabu nyingi barani Ulaya.

Lukaku amewahi kukitumikia kikosi hicho cha Blues msimu wa mwaka 2011 hadi 2013, kabla ya kuuzwa moja kwa moja katika klabu ya Everton na baadaye kutua Manchester United na hatimaye Inter Milan.

Chelsea wana kazi kubwa ya kupata saini ya Haaland, kwa sababu klabu kubwa kama Real Madrid, Barcelona na Manchester City nazo zimejitosa kuwania aina yake.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# KANE: HATIMA YANGU BAADA YA EURO 2020

Akili yangu kwa sasa inafikiria zaidi kile nitakachokifanya uwanjani hadi kipindi cha majira ya joto tutaangalia...

**LONDON, England**

NYOTA wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane, amesema ataamua majaliwa yake baada ya michuano ya Mataifa ya Ulaya, Euro 2020, inayotarajiwa kufanyika Juni mwaka huu.

Kane amekuwa akihusishwa na miamba wa Ligi Kuu England, Manchester United na Manchester City, pamoja na wababe wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Real Madrid.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ambaye aliibuliwa kwenye timu ya vijana ya Tottenham mwaka 2009, mkataba wake na Spurs unamalizika mwaka 2024.

Lakini Kane kwa sasa hataki kuzungumzia kuhusu hatima yake wakati akijiandaa na Tottenham kwenye fainali ya Kombe la EFL dhidi ya Man City mwezi ujao, huku England nayo ikipanga kuwania taji lake la kwanza kubwa la kimataifa tangu mwaka 1966 kwenye mashindano hayo ya Euro 2020.

**"Nafikiri hilo ni swali gumu kwa sasa," alisema Kane akiliambia gazeti la Telegraph wakati alipoulizwa kuhusu kelele zinazozagaa kutokana na majaliwa yake pale Tottenham.**

"Ni muhimu kwamba akili yangu inaangalia zaidi kwenye mechi za England zinazokuja na kuangalia kipindi cha msimu kilichobaki na mashindano ya Euro. "Kufikiria uvumi kutakufanya usiwe na wakati mzuri dimbani, hivyo hilo jambo kwa upande wangu kwa sasa silifikirii kabisa.

"Mara zote huwa nafikiria zaidi kwa jambo moja na hiyo ndio kazi yangu kubwa ili kumaliza kwa uimara zaidi nikiwa na Spurs, na pia kuisaidia England kushinda Euro na hilo ndilo lengo langu kubwa kwa sasa.

"Angalia, nitajaribu kukaa mbali na uvumi huu kadiri inavyowezekana na kujiweka mbali kabisa.

"Akili yangu kwa sasa inafikiria zaidi kile nitakachokifanya uwanjani hadi mwishoni mwa msimu huu, kipindi cha majira ya joto, na tutaangalia baada ya hapo."

Kikosi hicho cha Jose Mourinho, Tottenham kipo nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu, kikipitwa pointi tatu kutoka kwenye nafasi ya kufuzu michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

England imepangwa Kundi D kwenye mashindano ya Euro 2020 pamoja na Croatia, Scotland na Jamhuri ya Czech.

Kane amefunga mabao 17 kwenye Ligi Kuu msimu huu, huku akifunga 27 kwenye mashindano yote kwa Tottenham msimu wa 2020-21.

## KWA UFUPI

### ARSENAL NA ADA YA ODEGAARD
ARSENAL ina wasiwasi bei ya kumnunua Martin Odegaard inaweza kupanda hadi pauni milioni 50 kipindi ha majira ya joto, huku timu kama Chelsea, Liverpool na PSG znaweza kuingia kwenye mbio za kuwania saini yake. **(Star on Sunday)**

### MBAPPE KUTOA SITA MADRID
GARETH Bale anaweza kuwa mmoja kati ya wachezaji sita ambao Real Madrid itawauza ili kupata fedha za kumsajili nyota wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe mwenye miaka 22 na straika wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri miaka 20. **(Sunday Mirror)**

### ABRAMOVICH ATAJIWA HAALAND
KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, amemwomba mmiliki wa 'Blues' hao, Roman Abramovich, kumtumia mshambuliaji wa Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 25, kama sehemu ya kumsajili Erling Haaland kutoka Borussia Dortmund. **(Sunday Express)**

### STERLING NA MKATABA MPYA
MAZUNGUMZO ya kuhusu mkataba mpya kati ya winga wa Manchester City na England, Raheem Sterling na mwenye umri wa miaka 26 na klabu hiyo, yamesimama hadi kipindi cha majira ya joto. **(Star on Sunday)**

### MADRID HAIMTAKI TENA BALE
MSHAMBULIAJI wa Wales, Gareth Bale, hayupo kwenye mipango ya Real Madrid kwa msimu ujao, licha ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 31 kusema kwamba, anapanga kurudi katika klabu hiyo ya Hispania mwishoni mwa msimu huu, baada ya kumaliza muda wake wa kucheza kwa mkopo kule Tottenham. **(Marca)**

### MAN UNITED YAMTAKA SARR
MANCHESTER United wanaweza kufanya usajili wa winga wa Watford na Senegal, Ismaila Sarr mwenye umri wa miaka 23, badala ya nyota wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 2o, kama watashinda kumsajili Erling Braut Haaland kutoka kwa miamba hao wa Ujerumani. **(Sunday Express)**

### ADA YA LLORENTE YATAJWA
MANCHESTER City watatakiwa kulipa pauni 103 kama wanataka kumsajili kiungo wa Atletico Madrid na Hispania, Marcos Llorente mwenye umri wa miaka 26. **(Marca, via Metro)**

### ZIDANE KUAMUA KWA ODEGAARD
REAL Madrid watamuuza au kumtoa kwa mkopo kiungo wa Norway, Martin Odegaard mwenye umri wa miaka 22, ambaye anacheza kwa mkopo kule Arsenal, kama Zinedine Zidane atabaki kuwa kocha wa kikosi hicho. **(Football Insider)**

### CAVANI ATAKIWA BOCA
KOCHA msaidizi wa Uruguay, Mario Rebollo, amesema utakuwa msaada mkubwa wa timu ya taifa, kama Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 34, ambaye anacheza kule Manchester United, ataamua kujiunga na Boca Juniors. **(Sunday Mirror)**

### AGUERO AWANIWA INTER
KLABU ya Inter Milan itasikiliza ofa kwa ajili ya mshambuliaji wake, Romelu Lukaku raia wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 27, kama watafanikiwa kumsajili straika wa Manchester City na Argentina, Sergio Aguero mwenye umri wa miaka 32. **(Star on Sunday)**

HABARI MICHEZO

# BARAZA ATAJA SHIDA ILIPO KIKOSI CHA KAGERA SUGAR

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza, amesema ameridhishwa na uwezo wa mchezaji mmoja mmoja wa kikosi chake kutokana na kuongeza utulivu na kujiamini, jambo ambalo anaamini litawapa matokeo mazuri katika mechi za lala salama za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Baraza alisema amekabidhiwa timu hiyo na malengo yake makubwa ni kuanza kwa kuwajengea kujiamini wachezaji kutokana na uwezo mkubwa wa nyota wake hao.

Alisema kila mchezaji ana elewa timu iko katika wakati mgumu, lazima wapambane kutafuta matokeo katika mechi za nyumbani ambazo hawachezi kwa presha kubwa.

"Shida kubwa kwa sasa ni kujiamini, kwa kweli kipindi cha wiki moja nimekuwa na vijana hawa, kuna mambo mengi tumezungumza na kufanya mazoezi pamoja, kwa upande wangu vijana wamejaribu kujituma mno," alisema Baraza.

Alisema wiki hii moja haikuwa rahisi kwa kila mchezaji ila anashukuru vijana pamoja na benchi la ufundi walijitolea kwa moyo mmoja.

"Ligi ina ushindani mkubwa kila mtu ana matarajio yake, kwangu nahitaji kupata matokeo mazuri ili kuondoka katika nafasi tuliyokuwapo katika msimamo ambayo si nzuri kwetu," alisema Baraza ambaye amejiunga na timu hiyo wiki mbili zilizopita akitokea Biashara United, baada ya uongozi wa Kagera kumtimua Mecky Maxime kutokana na kutoridhishwa na mwenendo wa matokeo.

Alisema kikubwa ni wachezaji kufuata maelekezo na kufanya yale waliyokubaliana kwa kushinda kwenye ligi na kila mchezaji na timu kwa ujumla wanahitaji kupata matokeo chanya.

Kagera Sugar ipo katika nafasi ya 13, kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 18, baada ya kushuka dimbani mara 24 na kujikusanyia pointi 25.

**TUMEWASILI...**




Timu ya Taifa ya soka la Ufukweni ya Burundi ikiwasili Dar es Salaam jana tayari kwa ajili ya mchezo wa kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) dhidi ya Tanzania, utakaopigwa kesho katika Ufukwe wa Coco jijini Dar es Salaam. **PICHA: SAADA AKIDA**.

## Zanzibar Heroes, Matabeleland wapigwa kalenda

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), limeupiga kalenda mchezo wa kirafiki kati ya timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes) na timu ya Matabeleland, hadi Mei mwaka huu.

Mchezo huo awali ulipangwa kuchezwa Jumamosi Machi 27, mwaka huu, visiwani Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Meneja wa Leseni za Klabu wa ZFF, ambaye ni mratibu wa mchezo huo, Mbarouk Othman, alisema sababu za kusogezwa mchezo huo ni timu ya Matebeleland kuomba iwe hivyo ili kuepusha gharama za kuja Zanzibar mara mbili katika mechi ya kirafiki na kwenye michuano ya CONIFA Africa.

Alisema timu hiyo imeona kwa kuwa michuano ya CONIFA Africa Inafanyika visiwani hapa Mei, mwaka huu, hivyo ni afadhali mchezo huo wa kirafiki uchezwe mwezi huo pindi watakapowasiliana ili kujiandaa na CONIFA itakapotolewa tarehe ya kuchezwa mashindano hayo.

"Tumefanya nao mawasiliano na wenzetu wa Matebeleland na wao wameona bora mchezo huo uchezwe Mei pindi watakapokuja Zanzibar katika michuano ya CONIFA Africa, ili waweze kuepusha gharama na ZFF kwa pamoja tumekubali ombi lao," alisema.

Hata hivyo, aliwataka wadau wa soka Zanzibar kuendelea kutoa hamasa ya mashindano hayo ambayo yanatarajiwa kutimua vumbi mapema Mei mwaka huu huku Zanzibar ikiwa mwenyeji kwa mara ya kwanza.

# Azam FC bado na jambo lao Ligi Kuu, FA Cup

**Na Saada Akida**

BAADA YA kuanza mazoezi wakitokea katika mapumziko mafupi kupisha mazishi ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, uongozi wa Klabu ya Azam umesema mkakati wao ni kurejea kwa kasi kubwa katika Ligi Kuu Bara ili kuhakikisha wanafikia jambo lao walilodhamiria msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili Dar es Salaam jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, alisema malengo makubwa ya timu yake ni kupata matokeo chanya kwenye kila mechi watakayocheza ili kurudi kwenye nafasi itakayowafanya kutimiza malengo waliyojiwekea.

Alisema wanapenda kuona kwenye kila mechi wanapata matokeo chanya kwa kuwa malengo yao ni kufanya vizuri msimu huu ikiwamo kutwaa ubingwa wa ligi hiyo na Kombe la FA.

"Nina imani na wachezaji wetu kufanya vizuri kwenye michezo yetu yote iwe ligi na hata FA, kikubwa ni kuendelea kuwapa maelekezo na kuyafuata huku washambuliaji wakiongeza umakini kwa nafasi wanazotengeneza uwanjani.

"Ni muhimu sana kwa nafasi tunazopata kuhakikisha wanakuwa makini jambo ambalo tulianza kulifanyia kazi kabla ya mapumziko na tunaimani tunaenda kufanya vizuri na kuendeleza ushindani katika ligi," alisema Vivier.

Alisema licha ya kuimarisha safu ya ushambuliaji, pia wanaendelea kuhimiza safu ya ulinzi kuwa makini kwa kutoruhusu nyavu zao kutikiswa pindi wanapopata ushindi.

Azam FC kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ipo nafasi ya tatu baada ya kucheza mechi 24 na kukusanya point 44 wakati huu Yanga ikiwa kileleni na pointi zake 50 zilizotokana na kushuka dimbani mara 23, huku Simba iliyocheza michezo 20 ikiwa nafasi ya pili na alama 46.

Ligi hiyo ambayo iliyopo mapumzikoni kupisha Kalenda ya Fifa, inatarajiwa kurejea Aprili 6, mwaka huu kwa Biashara United kuikaribisha Polisi Tanzania huku JKT Tanzania ikiwa mwenyeji wa Mwadui FC na Azam FC ikiialika Mtibwa Sugar katika Uwanja wake wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

# Michezo

Jumatatu Machi 29, 2021

Nipashe


HABARI UK.20




## Messi, Ronaldo sasa watakiwa Marekani

## Ntibazonkiza awafunika nyota EPL mabao Afcon

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI timu ya Taifa ya Burundi, ikishuka dimbani nchini Morocco kesho kuwavaa wenyeji hao kwenye mechi ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) zitakazofanyika mwakani nchini Cameroon, mshambuliaji wa Klabu ya Yanga, Mrundi Saidi Ntibazonkiza, ndiye anayewakimbiza mchakamchaka washambuliaji wa Ligi Kuu Ulaya katika michuano hiyo.

Baadhi ya nyota wanaocheza Ligi kubwa barani Ulaya, wakiwamo Alex Iwobi anayeichezea Everton ya England na timu ya Taifa ya Nigeria, Vicent Aboubakari (Besiktas/Cameroon), Hakim Ziyech (Chelsea/Morocco) hadi sasa kila mmoja amefunga mabao matatu tu kwenye michuano hiyo ya kuwania kufuzu Afcon wakati Ntibazonkiza yeye ameshacheka na nyavu mara nne kabla ya mechi za jana.

Katika orodha hiyo ya wafungaji wanaongoza kwa mabao kwenye michuano hiyo ya kuwania kufuzu Afcon, wachezaji wengine wenye mabao manne sawa na Ntibazonkiza ni Victor Osimhen (Napoli/Nigeria), Percy Tau (Brighton & Hove Albion/Afrika Kusini) na Louis Mafouta (Neuchatel Xamax/Afrika ya Kati).

Ntibazonkiza atakuwa na nafasi ya kuongeza idadi hiyo ya mabao kesho wakati Burundi itakapoivaa Morocco ugenini ikihitaji ushindi ili kuungana na wenyeji hao ambao tayari wameshafuzu, huku ikiiombea Afrika ya Kati ishinde dhidi ya Mauritania ama itoke sare.

Katika kundi hilo la E, Morocco ipo kileleni ikiwa na pointi 11 ikifuatiwa na Mauritania yenye alama sita huku Burundi ikifuata na pointi zake tano na Afrika ya Kati ikiburuza mkia na alama nne mkononi.

PASUA NGOME...



Mshambuliaji na Nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, akijaribu kupasua ngome ya Libya kwenye mechi ya Kundi J ya kukamilisha ratiba ya kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana na Stars kushinda bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MSUVA AREJESHA FARAJA SAMATTA AKIKOSA MENGI

### ●●● Manula azidi kuwa shujaa Stars ikiwafuta majonzi Watanzania kwa kuichapa Libya huku...

**Na Adam Fungamwango**

BAO lililofungwa na Simon Msuva sekunde chache kabla ya kwenda mapumziko, limeifanya timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars kuibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Libya kwenye mechi ya kufunga dimba Kundi J, kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika zitakazofanyika mwakani nchini Cameroon.

Ilikuwa ni mechi ya kwanza kwa Taifa Stars kucheza kwenye ardhi ya nyumbani, baada ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli, aliyefariki Dar es Salaam, Machi 17 na kuzikwa Chato mkoani Geita, Machi 26, mwaka huu.

Msuva aliwapa faraja Watanzania alipounganisha mpira wa krosi akiwa katikati ya walinzi wa Libya, kutoka kwa Nicoson Kibabage. Msuva alikuwa anasahihisha makosa yake, baada ya kukosa bao la wazi akiwa yeye na nyavu dakika ya 25.

Nahodha wa Stars, Mbwana Samatta, aliwazidi mbio mabeki wa Libya na kumlamba chenga kipa Murad Al Wuheeshi, lakini mpira aliopiga uligonga mwamba na kurejea uwanjani, ukamkuta Simon Msuva ambaye alibaki yeye na lango, lakini shuti lake la mguu wa kushoto likatoka nje ya lango kwa mshangao wa wengi.

Katika mechi hiyo, Samatta alikosa mabao mengi ya wazi dakika ya 16, 25, 38, huku Ashi Manula akiendelea kuthibitisha ubora wake kwa kuokoa hatari tatu zilizoonekana kuwapa mabao Libya.

Pamoja na matokeo hayo, Stars imeshindwa kukata tiketi ya michuano ya AFCON mwakani, baada ya kumaliza Kundi J ikiwa na pointi saba, nyuma ya Equatorial Guinea yenye pointi tisa na Tunisia iliyomaliza kinara wa kundi ikiwa na pointi 16.

Wakati Tanzania ikimaliza kwenye nafasi ya tatu, Libya imekamata mkia ikiwa na pointi tatu tu.

Mechi iliyochezwa Alhamisi iliyopita ugenini dhidi ya Equatorial Guinea ndiyo iliyositisha ndoto za Watanzania kukata tiketi ya kwenda AFCON kwa kufungwa bao 1-0.

Kwenye mechi nyingine ya kundi hilo, timu ya Tunisia ikiwa nyumbani iliitwanga Equatorial Guinea mabao 2-1 kwenye mechi ambayo haikuwa na umuhimu wowote kwani timu zote hizo zimefanikiwa kutinga fainali hiyo itakayochezwa Januari na Februari mwakani.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

7708556 541002 >